


# YANTRA DHAMMA

MITAZAMO NA TAFAKURI: UTU, MBINGU NA NCHI



MTU USANISI


JF


Agosti, 2024

- Collective 'Intonation of Senses' and the 'Sensibilities'
- Individual/Collective social capacity for Self Determination

- Mfanyiko kumbaizi wa hisia tofauti tofauti na 'Kujisikia'
- Uweza wa kijamii wa mtu mmoja mmoja ama jamii kumbaizi kwa ajili ya 'Kujichagulia'

- Fanusi ya 'Mwangaza Dhahabu' kutegemea Taamuli ya Nuru ya Ufahamu
- Jamii katika 'Sovereini Jumuifu' kwa hali na Mali -- ridhiko, shukrani na kusifu 'Roho ya Uzima wote'
- Golden Light Function due to 'conscious Light of Enlightenment'
- Sovereign Integral Society in the state of Grace—Gratitude, thanks and Praise to the 'Spirit of all Life'.





## SEHEMU YA KWANZA: MAJENZI YA KAYA NA NYUMBA

Marejeo na 'Siku zetu'

Hatma ya 'Viriba vya Zamani' na 'Mvinyo Mpya'

Kujichagulia: Mashikizo kwa Shauku

Utaamuliko Jamii: Karata ya 'Dume la Shupaza' ilivyo ni Ufunguo wa 'Mapiku'

Gari la UTU: 'Safari ya Kiutamaduni'

Kutokea 13 na 33 ya Safari--Kumbukumbu la 'Miongozo'

Uskani wa Safari: Studio 'Utaamuliko Jamii' na 'Maendeleo'

Kitovu cha 'Dira ya Maendeleo' katika nasibu ya 'Utaamuliko Jamii'

Msafiri Kafiri: Mwenda Tezi na Omo...

Marejeo Ngamani: Kujisukanya na kujikung'uta mavumbi

Kila Mtu anauchukua Mzigo wake yeye Mwenyewe

Isemwavyo' Nira iliyo ni Nyepesi'

Mambo ya Mlimani: Muongozo kwa ajili ya Taamuli, Kazi na Ulinzi

Fimbo ya Musa: Miongozo kwa ajili ya ‘Udugu’ na ‘Haki’

Alama za Uchungaji: Muongozo wa Ulinzi na Malango ya UTU na Ustawi katika Kujichagulia

Mifumo na ‘Mafumbo ya Imani’ : Kukadirisha Jithada za UTU na Nyakati

## **SEHEMU YA PILI: FUNGUO ZA ‘MAARIFA YA KAZI’**

Metafizikia ya Mifumo: SASA-NIA ilivyo ni kitovu cha Ufahamu Mkuu na Uweza

Shika Neno, Tenda Neno: Ualama na Matendo kwa Wanajamii



Ualama Taasisi: Ufunguo kwa Maagano ilivyo ni ‘Upepo’ na ‘Maji’ wa UTU

Amerika hata Tanzania: Marejeo ya Nia na Misingi ya Nchi na Tawala

Uzao wa Mzabibu na ‘Ndoto ya Ujamaa’ wa kweli

Nyota ya Utimilifu wa Miundo na Mageuzi

Jua la Maarifu



# SEHEMU YA KWANZA: MAJENZI YA KAYA NA NYUMBA

## Marejeo na 'Siku Zetu'

ALRIGHT,

[[QUOTE: mose\(JF\)](#)]:

'Matrix' ni jambo lenye asili ya 'Kumbukumbu'...

Kwa hivyo hisia zako, kimuktadha akilifu wa uono na ufikirifu mifumo, ni sahihi...

Kumbukumbu ina 'unje' na 'undani'...

Matriksi, kiufundi, ni mambo ya metafo za 'Shetani' na '[Malaika](#)' na '[Kujichagulia](#)'...

Kwa hivyo 'Matriksi' katika sura na hadhi ya '[kumbukumbu utaasisi](#)' ni mambo ya '[miongozo](#)'...

Matriksi ni KUBU ya sura, hadhi na msimamo wa jamii kwa/katika 'mapana ya wakati/nyakati'...

Uhusiano wa KUBU na Mifumo ni mambo ya '[mafumbo ya imani](#)'...

Inaweza kuwa ni mchanganyiko wa 'lugha za wanadamu' na 'lugha za malaika', kwa ajili ya miongozo ya 'maisha, kuishi na kheri ya ustawi' wa jamii kumbaizi kwa daraja na utukufu fulani -- daraja na utukufu wenye kukusudiwa kwa jamii, viongozi, sura ya nchi na tawala...

Kwa hivyo, kumbukumbu zote huja na 'KUBU'--Kiufundi, mambo ya [Duara na Nukta](#)--'Mwezi na Nyota', vivyo hivyo 'Msalaba'...

Mambo ya '[Ontolojia ya Taasisi](#)'...

Hmmm

<https://www.youtube.com/watch?v=AqGthp56KfM>[/URL]

[/QUOTE]

Mapicha-picha...

[[QUOTE: Kaloo\(JF\)](#)]:

Nasi mpaka hapo,Yale Petro aliyoyasikia mlimani juu ya kujenga vibanda vitatu,Eliya,Musa na Yesu Kristo yameshakwisha kusemwa kwa Mwana wa Adamu aliyezoezwa kupambanua ya Sirini na Mungu wake aliyomtuma kwetu(wakina-Petro baada ya jogoo kuwika majira yote Ni vile vile).

**N:B** Movement in Space and time is **Elohim Jivah**.

**Mungu ni mmoja**,mjumbe ni katika mabonde na miinuko

Nimemtuma njiwa, **kwenu Alete salamu** .

[/QUOTE]

NKNS...

'Mambo ya Nyakati' ni nuru na utukufu wa fahamu kumbaizi ya jamii na 'ma-jua ya ufahamu' katika mila, desturi na tamaduni yeyote kisomoni.

- Elohim Jivah--[Miungu duniani](#) katika [Miili ya Kuja na kwenda](#)...  
Mambo ya Supasha-Wakati, kng: Space-Time.

- [Sanduku la Agano](#) lililo ni Ushindi kwa Taifa ni mambo ya '[KUBU na Mifumo](#)' katika '[mafumbo ya Imani](#)'...

Kwa minajili ya haya mawili, Elohim Jivah ni habari za 'marejeo ya watu wa kabila Ndege'--watu wa 'mafumbo ya imani'.

Watu wa 'kabila ndege' walipata kusema kuwa 'watarejea'--kurejea kwao ni kwa ajili ya 'kuimalizia shughuli'; shughuli hii ni mambo ya 'Imani, Tumaini na Upendo' kwa vizazi--vizazi vya wanadamu.

Namna ya kurejea kwa 'watu wa kabila ndege' nayo yamekuwa ni habari za 'mafumbo ya imani'...

Mambo ya 'Mafumbo ya Imani' yanaweza 'kubanguliwa' ukweli wake kwa ELIMU 2.0 na ELIMU 3.0.

Elimu 2.0 ni 'Uono na Ufikirifu Mifumo' na ELIMU 3.0 ni 'ILIMU ilivyo ni metafizikia ya Elimu'.

Elimu 1.0 ni mawanda yote ya maarifa yatokanayo na fahamu za mwili, kumbukumbu/uzoefu wa vina vya tafsiri vyenye ukomo -- mambo ya maarifa ya 'Kawaida' ambavyo mtu/mwanajamii ananasibika na 'kujua mambo kwa sehemu' kulingana na 'visomo' vya 'elimu dunia'.

Elimu dunia ndiyo basi yaweza kuwa si lolote bali jukwaa la maridhiano ya utambuzi na ufahamu kwa mambo ya jamii--kisura ya nchi, tawala na utukufu wake; elimu rasmi ni shughuli ya kutengeneza 'watawala' na 'watawaliwa' kufaa 'mifumo' ya hali, sifa na daraja la utamaduni na ustawi wake; wenye kuzungumza hili kwa ugha ya kiingereza wanalitaja kana '[Status Quo](#)'...

'Statusi Kwou', ndiyo zao la taasisi, matendo yake na nyakati; ambavyo haya ndiyo hasa hufanya 'Mifumo' katika jamii. Jinsi shughuli ya elimu ilivyo--kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vikuu, ni shughuli ya 'kuwatengeneza' watu kiakili ili wafae katika dunia ya 'wajanja'--Ujanja ni 'kuwahi'; halafu ndiyo 'kupata'... Aliyewahi ndiye 'muamuzi' wa mwenye kupata ama kukosa baada yake...

'Statusi Kwou', ndiyo zao la taasisi, matendo yake na nyakati; ambavyo haya ndiyo hasa hufanya 'Mifumo' katika jamii; Jinsi ya wenyekupata na wenyekukosa kudumu pamoja ni mambo ya utundu wa kuzitengeneza 'kawaida' na kuziua kwa wanajamii.

Wanajamii ndiyo wanaoridhia KUBU na Mifumo kwa hali zao--iwe ni kwa raha ama karaha wakati mmoja hata mwingine. Kwa mintarafu ya hili, kinachoweza kuibadilisha 'statusi kwou' ni namna ingine ya 'maarifa' na mbinu za kukadirisha haya maarifa--Uono na ufikirifu mifumo...

=====

[https://www.youtube.com/watch?v=xBui-1Ic2vs&list=OLAK5uy\\_nCDlDD-JSYoNarRu3gY4TW8Bs1JGrYVQI](https://www.youtube.com/watch?v=xBui-1Ic2vs&list=OLAK5uy_nCDlDD-JSYoNarRu3gY4TW8Bs1JGrYVQI)

=====

### **Hatma ya ‘Viriba vya Zamani’ na ‘Mvinyo Mpya’**

'Statusi Kwou', ndiyo zao la taasisi, matendo yake na nyakati; ambavyo haya ndiyo hasa hufanya 'Mifumo' katika jamii; Uono na ufikirifu mifumo ni jambo lenye kukadirisha uweza wa kiutambuzi katika kung'amua asili ya (1) dhamiri, (2) fikra/wazo/vina vya tafsiri ya ubayanifu wa mambo na (3) Mifumo--hatma ya udhibiti kwa 'kujichagulia' na 'matendo' kupitia ufanyaji maamuzi/uchaguzi wa 'mapenzi ya kuishi' ndani ya mseto wa jamii. Kwa mintarafu ya hili, Uono na Ufikirifu Mifumo ndiyo khasa daraja la kiutambuzi linaloweza kuleta 'mapinduzi' ama/na 'mageuzi' ya kijamii kulingana na 'Nuru ya Ufahamu' katika mwanajamii...

Utamilifu wa uono na ufikirifu mifumo miongoni mwa wanajamii ndiyo jambo linaloweza kuja kukadirisha 'Sovereini Jumuiifu'. Kontrasiti ya Nuru ya Ufahamu yenye kutofautiana/kutolingana miongoni mwa wanajamii ndiyo huzaa mambo ya 'mahusiano ya kinguvu' miongoni mwa wanajamii na pia kusababisha 'vuta-nikuvute' ya kukadirisha migongano ya 'maslahi binafsi ama/na maslahi jamii'... Kwa mintarafu ya hili, wema na ubaya/uovu wa jamii/wanajamii ni mtanzuko wa kimaadili; vivyo hivyo kukosa

vitovu ingilianifu vya nia na mapenzi ya jamii. Hili ndilo asili ya 'dini' na 'dola' kuwa 'maslahi' ya pamoja... Kwa kuwa dola huhitaji 'nchi kutawalika' na hali dini hutafuta jumuiya za kiimani kwa minajili ya maadili, utaratibu na mwenendo wa kimaisha...

Dini na Dola, ni wadau wa kukadirisha 'Statusi Kwou'--katika lugha ya elimu ya jamii, hili linaweza kutajwa kama '[wadau](#)' wa 'amani ama/na utangamano' wa nchi na tawala...

Udau wa amani na utangamano wa nchi na tawala ni ujuzi na ufundi unaohitaji 'Uono na Ufikirifu Mifumo' ili kujenga upeo wa kuyaona 'ya ndani' na 'ya nje' ya jamii; vivyo hivyo ya 'wakati huu' na ya 'wakati ujao'... Jambo hili ndilo hukadirisha mashauri ya 'Usalama wa Jamii/Taifa/Dola/Himaya/Ukoo' n.k Kwa mintarafu ya hili, ulimwengu wa leo '[umekopa](#)' mengi kwenye umahiri wa mashirika/Taasisi za kidini ili kusuka USASA wa jamii katika sura na tawala ya tuseme 'Dola' ama/na 'Himaya'... Mashirika/Taasisi za Kidini '[ndiyo moyo na akili ya ndani](#)' mataifa mengi duniani--labda karibia yote tu.

‘Taasisi za Dini’ na ‘dini’ kwa Ujumla ni mambo ya Elimu 3.0... Kwa hapa Tanzania, Mwanajamii hujinasibu na Elimu 3.0 kwa namna isiyo moja kwa moja--'Mwenge wa Uhuru' kwa mfano ni utaasisho wa 'mafumbo ya imani' katika [USASA](#) wa jamii ya leo. Kwenye Ususi wa taifa jipya, dola na maagano ya mapito ya kimageuzi jamii kwa ajili ya 'Taifa Kubwa', Afrika, mwenge wa Uhuru ni fumbo la imani kwa ajili ya '[Utaamuliko Jamii](#)'. Kwa mintarifu ya hili, ‘utaasisi wa mwenge wa uhuru’ ni shughuli ya 'ukumbusho' wa jamii 'kuamka' na kuinuka juu ya yote ya maendeleo na ustawi wao. Hili ndilo msingi wa 'Miinuko, Mlima/Mlima na Kusimika 'Mwenge wa Uhuru'--Mwenge wa Uhuru juu ya Mlima Kilimanjaro...

=====

[https://www.youtube.com/watch?v=BODwWQzQ9O8&list=OLAK5uy\\_nCDlDD-JSYoNarRu3gY4TW8Bs1JGrYVQI&index=8](https://www.youtube.com/watch?v=BODwWQzQ9O8&list=OLAK5uy_nCDlDD-JSYoNarRu3gY4TW8Bs1JGrYVQI&index=8)

=====

## **Kujichagulia: Mashikizo kwa Shauku**

Maagano, ni muktadha wa mkataba kati ya 'Watawala na Wataliwa' ambavyo mashikizo ya dola na raia kiwajibu, vitendo na dhamiri kudadavuliwa bayana--KATIBA. Kwa nchi ya Tanzania, hili huanza muktadha wa 'Duara na Nukta' la 'Mipaka ya Nchi' na 'Dhamira kuu'--kujenga nchi ya watu wenye UHURU, UDUGU, HAKI na AMANI. Yumkini mataifa mengine mengi hujidadavua kwa haya haya; lakini tofauti ya Tanzania na hayo mataifa mengine ni 'Rasilimali Watu' wenyewe, kwa minajili ya 'Viongozi Waasisi' na 'Mazingatio ya Dola' yenyewe katika misingi ya haya.

Habari za maagano zina asili ya mambo kama kwenye kisa cha Musa na wana wa Israeli...

Maagano huja na 'Jinesesia' ya madhahiriko--namna ambavyo jamii hujitukiza kutoka usikitu na kuja kuwa kitu--Ontolojia ya Taasisi. Jinesesia ya Taifa kwa mfano, haina tofauti na ile ya miili ya viumbe hai; kwa Tanzania, jinesesia yake ni 'Uchotara' wa jamii mbalimbali kwa namna za makabila ya wenyeji, wahamiaji wa kuja na ukoloni na kifuatiacho ukoloni huo. Kwa hivyo taifa la Tanzania lina ujinjetifu wa unasaba, dini na utamaduni ulio ni chotara.

Elimu 3.0 ndiyo inaweza kumpatia mwanajamii ufunguo wa ufunuo kuyafahamu ya jana, leo na kesho kuhusiana na jamii--uzima wa 'wakati-jamii-machaguo ya kitaasisi-matukio'. Kwa mtu wa Rizayati ya Elimu 3.0; uwezo hufanyika kukadirisha uono na ufikirifu mifumo wa 'Jaala' ya jamii. Kwa hivyo maisha ni 'kumbukumbu hai' la miongozo ya mila, desturi na utamaduni wa jamii yeyote kisomoni. Kwa mintarafu ya hili la 'kumbukumbu hai', hili ndilo hukadirisha 'Unje' na 'Undani' wa Matriksi ya Jamii.

Kwa Tanzania kwa mfano, sanduku lake la agano, imepata kuwa ni 'mbegu' ya 'Yantra Dhamma'--ambavyo 'Jaala' yake ni kuja kuwa ni nchi ya 'Kuanza Nia' katika makuu ya tawala ya Nchi, Utamaduni na Ustawi--kuwa nchi ya 'Mwanzo' na tena nchi ya 'KUTOKA', nchi ya HESABU; nchi ya 'Mambo ya Walawi' na zaidi 'Kumbukumbu la Miongozo'. Kwa mintarafu ya haya 'Wafalme' na 'Waamuzi' katika dunia ya leo ni mambo ya 'Dola' na 'Taasisi ndani ya Taasisi'. Ulimwengu wa leo hatuna 'Wafalme' bali tuna 'Maraisi na Taasisi Urais'. Marais na Taasisi ya Urais ni mambo ya Nyumba, na watu wa Nyumba... Waamuzi, ulimwengu wa leo ni shughuli ya wadau wa 'UTU' na 'UFUNUO'--kwa namna isiyo ya moja kwa moja...

=====

[https://www.youtube.com/watch?v=Y-fDOGuW8Lw&list=OLAK5uy\\_nCDlDD-JSYoNarRu3gY4TW8Bs1JGrYVQI&index=7](https://www.youtube.com/watch?v=Y-fDOGuW8Lw&list=OLAK5uy_nCDlDD-JSYoNarRu3gY4TW8Bs1JGrYVQI&index=7)

=====

**Utaamuliko Jamii: Karata ya ‘Dume la Shupaza’**

**ilivyo ni Ufunguo wa ‘Mapiku’**

UTU na UFUNUO ni mambo ya mfano wa ndege [Tausimoto](#) na tena habari za watu wa 'kabila Ndege'--[Wafanyambawa](#)... Kutoka uchina

ndiyo tunaweza kupata seti moja ya mfano kwa ajili ya '[muktadha wa vina vya tafsiri](#)' kwa muktadha akilifu wa uono na ufikirifu mifumo kuhusiana na [mafumbo ya imani ya utu](#)--utu na 'kode moto' za Joka/Dragoni katika ulimwengu wa '[Kujichagulia](#)'.

Yantra dhamma, [chombo cha Dhamma](#), ni ukadinali wa jamii katika 'Sovereini Jumuifu'. Kile ambacho ulimwengu wa kileo, fikra za karne ya 19 na 20 juu ya 'Ujamaa ama/na Usoshalisti' vimekuwa ni mbegu ya jambo lenyewe hasa--'Utaamuliko Jamii' utokanao na misingi ya UHURU, UDUGU, HAKI na AMANI.

Hapa Tanzania, jitihada zimefanyika, zinafanyika na zitaendelea kufanyika ili kutimiliza mageuzi kamili ya kijamii kwa ajili ya jamii yenye sifa, hadhi na daraja/utukufu wa 'Sovereini Jumuifu'. Dhamma ni uisho wa maisha kwa msingi ya mafundisho ya Siddhartha 'Buddha' Gautama—mtu mkuu aliyepata kuishi duniani takriban miaka 2600 iliyopita.

Mafundisho ya Buddha yana asili ya 'Gurudumu' na 'Mraba'--viwili vya 'Uisho wa UTU'; Funguo za 'Nuru ya Ufahamu' kupitia AKILI, UTAMBUZI na FAHAMU; ambavyo Buddha alitaamulika kuyafahamu ya Ulimwengu wote Mzima na basi kutengeneza msingi wa 'Miongozo' ya 'Utaamuliko' kwa wengine wote wenye kutafuta 'WONGOFU' kupitiliza mafumbo ya Uzima na Miili na Ufahamu. Miongozo hii ndiyo inayofanya asili ya 'Gurudumu Dhamma' na 'Njia ya Buddha'—Dhammapada.

=====

[https://www.youtube.com/watch?v=alnY2sy9\\_fk](https://www.youtube.com/watch?v=alnY2sy9_fk)

=====

## **Gari la UTU: ‘Safari ya Kiutamaduni’**

‘Gurudumu’ na ‘Mraba’, karne hii ya 21 ndiyo mapelekeo hasa ya ‘Yantra Dhamma’ na ‘Trizaniamu’. Kiufundi, katika [Gurudumu la Dhamma](#) kuna shauri la ‘[Utatu](#)’ wa (1) dhahiri, (2) fikra/matendo/nia katika ‘Imani Moja’ na (3) Mifumo—Mambo ya kujihifadhi/kukimbilia katika ‘Hazina’ ya vito thamani vitatu vya Ubuddha—Buddha, Dhamma na Sangha. Ulimwengu wa leo, haya ndiyo asili ya ‘Ontolojia ya Taasisi’ ambavyo ‘Muundo, Kujisikia na Ushawishi’ ndiyo kiini cha UTU na KUJICHAGULIA. Mraba, ni jambo la kielelezo cha ‘Muundo’ ambavyo ‘Miongozo’ ni nguzo ya imani kwa ajili ya fizikia na metafizikia ya jambo/mambo...

Buddha, katika Utaamuliko, alikadirisha ‘kode za utambuzi’ kuhusiana na maisha ya mtu katika ‘mapana ya wakati’--mapana ya wakati ni mapana ya supasha hapo hapo. Hili ndilo msingi wa Buddha na mafundisho ya ‘[Kweli Nne za Tunu](#)’; na basi hizi katika karne hii ya 21 ndiyo tunazungumza asili ya maisha ya mwanadamu kuwa ni ‘Mraba ndani ya Duara’--Yantra Dhamma ni ufunguo wa rizayati ya Elimu 3.0 ambavyo ‘Unje-Ndani’ wa ‘Kweli Nne za Tunu’ ndiyo (1) Dhukka, (2) Samudaya, (3) Nirodha na (4) Marga katika kupinduliwa ki-picha ya tafsiri.

Buddha, katika Utaamuliko, alikadirisha ‘kode za utambuzi’ kuhusiana na ‘maisha ya mtu’ kwa ‘Duara na Kitovu/nukta’ cha muktadha wa kadiri ya ‘uono na ufikirifu mifumo’ ilivyo ni mashauri ya ‘Samsara’ na ‘Maya’. Kwa mintarafu ya haya mawili, (1) fahamu, (2) uono na (3) vina vya tafsiri kuhusiana na yote, [yaliyodhahiri katika fahamu za kimwili na hata yale yanayopitiliza fahamu tano za mtu](#), ni ‘[maruweruwe-Maya](#)’ katika bahari ya ‘uzima

wa miili’. Basi yawa, [Samsara ni hatma za UTU ufanyikao na ‘miili katika uzima’](#).

Buddha, katika Utaamuliko, alikadirisha ‘kode za utambuzi’ ambavyo usifa-akili hu-**tatu**-sha mapana ya (1) mtenda, (2) kitendo na (3) jambo. Kwa mintarafu ya hili, uono na ufikirifu mifumo ndiyo intelijensia ya yote—mambo ya dhahiri na isivyodhahiri ya ‘tukio’. Hili lafanya meza ya ustawi wa jamii, kiufundi, ni mraba wa ‘Wakati-Jamii-Machaguo ya Kitaasisi-Matukio’. Ili kuweza kumudu fasaha ya uono na ufikirifu mifumo, ndiyo hubidi ‘mwanakisomo’ awe ni mtu wa ‘[vipassana](#)’, Basi ndivyo alama ya ‘UONO’ katika TRIZANIAMU ni mfano wa gurudumu la dhamma – gurudumu la dhamma pasi ‘duara’--[midenge minane](#)...

Midenge minane, kiufundi, ni ‘misalaba miwili’ yenye kushiriki kitovu kimoja—asili ya Nuru ya Ufahamu kuakisika katika ‘Miundo’...

Samsara na Maya, katika Trizaniamu, ndiyo asili ya ‘[Jicho Mashoto la Horasi](#)’ kuwa ndani ya miduara miwili—wa ndani na nje katika mahusiano ya fizikia na metafizikia ya mambo; tena basi kufanya ‘ukadinali/msalaba’ wenye kutengenisha UNNE wa (1) SUPASHA, (2) WAKATI, (3) MAADA na (4) NISHATI; akitipu ya ‘miundo na miongozo’ ya vyote. Kwa mintarafu ya haya, kisomo cha fizikia na metafizikia ya yote katika Ulimwengu, yaliyo dhahiri na yasiyo dhahiri, ni uwezekano kupitia ‘Uono na Ufikirifu Mifumo’.

Samsara na Maya, katika Trizaniamu, ndiyo asili ya ‘[Jicho Mashoto la Horasi](#)’ kuwa ndani ya miduara miwili ambavyo ‘Uzima wa Miili’ yote ni ‘Muziki’ wa ala za ‘Sauti za Kiufahamu’. Kwa mintarafu ya hili, asili hasa ya ‘WAKATI’ ni duara/tufe—vivyo hivyo SUPASHA.

Hivyo basi ‘Matukio’, kiufundi, ni ‘Ala’ na ‘Muziki’ katika ‘Intrigi za Ufahamu’ wenye kufanyika ‘Dhahiri’. Tena yawa, ‘Miundo yote’ huja na ‘Mifumo’ ya ‘Utonali wa Hisia’ kukadirisha uakilifu wa KUJISIKIA katika UTU.

Samsara na Maya, katika Trizaniamu, ndiyo asili ya ‘[Jicho Mashoto la Horasi](#)’ kuwa ndani ya miduara miwili ndiyo asili ya KUBU ya matriksi zote katika Ulimwengu dhahiri na usiyodhahiri kwa fahamu za ‘miili ya uzima’--katika mapana/vina visivyokuwa na mwisho vya ‘Uhuru wa Roho ya Uzima’ wote. Kwa mintarafu ya hili, ‘matukio’ na ‘Jinesesia’ ni ‘Ontolojia ya Taasisi’ kwa ‘asili-dhahiri’ ya mifumo ya (1) Mwangaza/Nuru, (2) UPEPO, (3) MAJI na (4) NCHI/ARDHI/MBINGU YA CHINI...

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=OjDi5NajUy8>

=====

### **Kutokea 13 na 33 ya Safari: Kumbukumbu la ‘Miongozo’**

Ukadinali wa Nuru, Upepo, Maji na Nchi ndiyo asili ya ‘Sanaa’ na ‘Alama za Kiutamaduni’ kwa mataifa ya watu Duniani na Taasisi za ‘UAHADI’/‘MAAGANO’-- ‘Dola’ na ‘Unchi/Taifa-Dola’. Mintarafu ya shauri/mashauri ya haya ndiyo karne hii ya 21 yanajitokeza kama ujumuifu wa (1) Msalaba wa matanuko yasiyo ukomo, (2) ‘Mwezi Mchanga’ na ‘Nyota’, (3) Mboni ya ‘Ajna’ na (4) Swastika ya ‘Mageuzi ya Utukufu’. Ujumuifu wa alama za ‘Intrigi za Ufahamu’ ndiyo ufunguo wa ‘Miongozo’ ya ‘Upana na Urefu, na kimo na kina’ kwa ajili ya ‘Utaamuliko Jamii’.

Afrika Mashariki ndipo mahala panapofanyika patakatifu kwa ajili ya ‘utaamuliko Jamii’ na ‘mbegu ya utaamuliko Jamii’. Kwa

mintarafu ya hili, jamii yoyote kisomoni, watu wake ndiyo wenye kufanya ‘Sura na Mienendo’ ya ‘Uweza, Nguvu na Utukufu’ wa UTU wake jumuiifu. Kiufundi, ‘idadi ya watu’ kufungamana na ‘hisia, ujuaji na kujisikia’ ndiyo hukadirisha ‘Mapana ya Jamii’ yenye Sura, Hadhi na Daraja la Ubora wa ‘Mwangaza’ wa ‘Uweza, Nguvu na Utukufu’. Kwa hivyo misingi ya Maendeleo ya Utu ni fumbo la imani juu ya mustakabli wa Kiroho, Maadili na Miiko.

Kwa Tanzania, kwa mfano, fumbo la imani kwa mustakabli wa Jamii kumbaizi ya ‘Taifa la Watanzania’ ina dhamira za (1) UHURU, (2) UDUGU, (3) HAKI na (4) AMANI. Tunu hizi nne za Utaifa zina mahusiano ya moja kwa moja na ‘Kweli Nne za Tunu’ za Buddha. Mintarafu ya hili, (1) ‘UHURU na AMANI’ ni mambo ya ‘Mbingu’ na hali (2) ‘UDUGU na HAKI’ ni mambo ya ‘Nchi’. Na basi, (3) ‘SURA ya NCHI na TAWALA’ na (4) ‘HAMASA ya UJAMII’ ni mambo ya ‘MKONO wa KUSHOTO na MKONO wa KULIA wa ‘UWEZA, NGUVU na UTUKUFU’ – Uweza, Nguvu na Utukufu katika fizikia na metafizikia ya ‘UTU na UZALENDO’.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=X74JArLOCJE>

=====

## **Uskani wa Safari:**

### **Studio ‘Utaamuliko Jamii’ na ‘Maendeleo’**

Utu na Uzalendo una mitihani ya ‘maisha’ na ‘kuishi’... Mambo ya (1) Dhukka, (2) Samudaya, (3) Nirodha, na (3) Marga.

Buddha alifundisha habari za ‘[Dhukka](#)’ ilivyo ni utostabali katika kupata/kuotea usahihi wa ‘vina vya tafsiri’ juu ya dhumuni ama/na madhumuni ya kuishi, kutafuta na kupata—[kubabaishwa na ukosefu wa ‘vitovu’ vya kubayanisha utimilifu wa ‘fikra na hisia’ zijazo na ‘miili ya nyama’](#) kwa ajili ya kuweza kubaini ‘hatma’ ya/za

mahangaiko yasiyo na ukomo katika (1) Dhamira, (2) Vina vya Uono na Utafsiri wa Mambo -- katika mafikara/mawazo, na (3) Harakati/Pilika za ‘Utaasisi’ na ‘Ontolojia ya Taasisi’ na ‘Mifumo’—‘Mambo ya Nyakati’. Kwa mintarafu ya mashauri haya, [Samsara](#) na [Maya](#), inaponza wote wenye (1) Usentienti/Kujisikia, (2) Udhamirifu wa Jema/zuri ama/na Ovu/baya, na (3) Nuru ya Ufahamu kupitia ‘Uzoefu wa Maisha’ kwa ‘[Gurudumu la Bahati ama/na Mikosi](#)’. Maisha ni ‘Tega Nikutege’ ya Nia na Dhamira katika ‘Mawazo na Matendo’ ya UTU, kuzaa ‘Mwiba’ wa maumivu, raha na karaha ya ‘Uisho’.

Buddha alifundisha habari za ‘[Samudaya](#)’ ilivyo ni Hamu ya Maisha inayomsababisha mtu kutwaa mwili kwa ajili ya ‘matamano’ ya kuishi na kustawi kulingana na ‘Kujijenga kwa Wazo-Utu’--‘Mhimili wa Nia’ kwa ajili ‘Kuwa’ ama/na ‘Kuja Kuwa’. Kwa mintarifu ya hili, ‘utwaaji mwili’ ni jambo lenye asili ya kupitiliza ‘kuzaliwa na kufa’ kwa kuwa ‘[fikara la wajiwazia utu](#)’ ni mbegu ya ‘Miili ya Uzima’ zaidi katika ‘Supasha-Wakati’. Kwa hivyo ‘Mhimili wa Nia’ ndiyo ‘nguzo ya imani’ ambavyo ‘Shika Neno, Tenda Neno’ ndiyo utaratibu (1) kuishi, (2) kujidhihirisha na (3) kukuwa/kuja kuwa ‘mtu hivi’ ama ‘mtu vile’.

‘Matamano’ na ‘wakati’ na ‘Matukio’ ndiyo asili na msingi wa jiometria ya utendekavyo (1) maamuzi, (2) kuchagua, na basi (3) ‘Kujichagulia’. Hivyo basi, ngozi ya meza ya ustawi wa mtu ama jamii inawambwa kwa mapana na marefu ya ‘wakati—jamii/mwanajamii--machaguo ya kitaasisi--matukio’. [Kumbukumbu Utaasisi](#) ni muktadha wa KUBU/Matriksi ilivyo ni mahusiano ya ‘miundo’ na ‘Mifumo’ ya Maisha kuweza kuathiri jiometria ya utendekavyo maamuzi, kuchagua na basi ‘Kujichagulia’ kwa wema ama ubaya -- wakati mmoja hata mwingine; fikara lolote kwa asili ni ‘Kumbukumbu/Matriksi’, matriksi ndiyo utawala wa kimaifara unaoweza kudumisha ‘fikara la kujiwazia utu’ katika

‘Isho’ moja hata jingine kwenye Supasha-wakati. [Isho moja na hata mengine ndiyo muktadha wa kuja na kwenda kwa ‘miili ya uweza’...](#)

Buddha alifundisha habari za ‘[Nirodha](#)’ ilivyo ni ‘[Nishani ya/kwa UTU BORA](#)’ katika [kujichagulia](#) ‘nia sahihi’ --Nia Sahihi katika ‘Uweza’ kwa ajili ya kupitiliza mitihani ya maisha na uisho kwa misingi ya ‘[Uono na Ufahamu](#)’. Kwa mintarafu ya haya, ili kumalizana na mitihani ya maisha na uisho kubidi kuzingatia ‘muenendo wenye kujikana nafsi’ katika UTU; kwa kuwa nafsi ndiyo muambata wa ‘[Dhukka](#)’. Basi ndivyo, [ufunguo wa nuru ya ufahamu katika njia ya Buddha](#) ni ‘[Gurudumu la Midence Minane](#)’; ambavyo Dhammapada ni ‘Uisho’ wenye dhamira ya matatu katika moja—[Vito Thamani VITATU vya UTU BORA](#).

Kwenye Nembo ya Taifa ya Tanzania, kwa mfano, Nishani ya/kwa UTU BORA inakuja kwa alama-jadi ya ‘Mkuki wa Jaaala’.

Kiufundi, ‘ukatikati wa mkuki wa Jaaala’ ni uakilifu wa mizania ya ‘mambo ya mkono wa kushoto’ na ‘mambo ya mkono wa kulia’ wenye kushinda ‘mapambano yote ya vile vyenye kuleta uhasimu ama mikangamo’ – uhasimu na mikingamo katika uwepo wa mtu/UTU katika maisha. Njia ya Buddha ni [Usahihi wa Katikati ya yote, kokote na mote](#). Kwa mintarafu ya haya, kwenye Yantra Dhamma, asili ya (1) [UONO](#), (2) mizunguruko: SURA NA MIENENDO YA JAMII; huja na alama za (3) ‘MBONI AJNA’ na ‘SWASTIKA’ katika (4) ‘MIONGOZO’ ili kukatidirisha (5) VINA-MAREFU-MAPANA-KIMO ya ‘Kitovu’ cha ‘Nishani ya/kwa UTU BORA’.

Kiufundi, Kitovu cha ‘Nishani ya/kwa UTU BORA’ ndicho khasa kile ‘kitovu OX’ cha ‘Kujitambua’ katika fremu kazi ya Uono na ufikirifu Mifumo—Trizaniumu. Kwa mintarafu ya hili, Trizaniumu ni ufraktali ya ‘pembetatu zipatazo tano(5)’ na si nne(4) kama

inavyoweza kuonekana kwa juu juu. Basi ndivyo pembe tatu ya tano ni UTATUSHO wa nukta tatu: OX-OY-OZ – mapelekeo ya (1) Wakati, (2) Kumbukumbu-Uzoefu, na (3) Jaala. Tena basi, haya matatu ndiyo hukadirisha matatu yaliyo ni (1) JAALA ilivyo ni mambo ya kuja na kwenda kwa ‘[miili ya uweza na kutenda](#)’, (2) MATUKIO ilivyo ni ‘Mambo ya Nyakati’, na (3) KUMBUKUMBU-UZOEFU ilivyo ni Mafikara ya Kujiwazia UTU katika ‘supasha-wakati’.

Kiufundi, ‘Nishani ya/kwa UTU BORA’ ni ALMASI ya DHAMMA; ambavyo ‘Nyota ya Daudi’ ni muingiliano wa Mambo ya Mbingu na Nchi ili kufanya utimilifu wa ‘Uweza, Nguvu na Utukufu’ kwa MAPANA-MAREFU-KIMO-KINA ya KUWA ama/na KUJA KUWA. Kwa mintarafu ya hili, TRIZANIA ni muktadha akilifu wa (1) MTENDA, (2) KITENDO na (3) FAHARI YA DHAHIRI/DHAMIRI YA KUJICHAGULIA. Basi ndivyo yaja kuwa UTU na UZALENDU ni ‘fumbo la Imani’ katika ‘Mchakato wa Mageuzi’ yasiyo na mwanzo wala mwisho ya (1) UTU, (2) UZIMA WA MILELE na (3) MADHAHIRIKO.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=pdzox6SI9H8>

=====

### **Kitovu cha ‘Dira ya Maendeleo’ katika nasibu ya ‘Utaamuliko Jamii’**

Mchakato wa Mageuzi ndiyo mambo ya ‘KUTOKA’ na ‘SALA’-- Mambo ya Kuuchukua Msalaba wako mwenyewe hadi ‘GOLGOTHA’. Kwa mintarafu ya muktadha akilifu wa namna hii, ‘Ishara ya Msalaba’ ni fumbo la imani kwa (1) JICHO LA UPAJI— Kitovu cha ‘Mbingu ya Sita’ ya utukufu wote wa UTU: Mambo ya

‘MBONI AJNA’ kuelekea UTUKUFU WOTE wa MBINGU, (2) MOYO—Mambo ya Kujitoa katika UTUMISHI kwa ajili ya ‘MAPENZI MEMA’ kuelekea/kujielekezea kwenye ‘Mapana ya Nchi yote’, na (3) Mkono wa kulia na kushoto/Upande wa Kulia na Kushoto wa ‘Mbawa za Dhamira’ ya Kustawi Juu na Chini ili ‘kuzijaza mbingu na nchi’ kwa Utukufu wa Roho ya Uzima wote...

VIPASSANA ni SALA; ambavyo ‘Hekima’ hufanyika katika UTU... Hekima ni Uweza wa kupambanua mambo ya fahari ya mbingu na nchi katika jicho la akili na uakilifu na tena katika muktadha wa ugani wa Moyo Mkuu wa kusikia na Kujisikia. SALA ni jambo lenye asili ya matatu (1) Kuwa kimya kiakili na fahamu ili ‘kusikiliza ya Moyo’ katika usafi wa dhamiri na mapenzi mema, (2) Kudhamiria Usahihi wa katikati katika nia, matendo na huduma ya UTU na Mapenzi mema, na (3) Kuwa na kiasi katika yote kwa kutambua uhitaji wako na wa wengine wote wenye kushiriki uzima, kusudi na haki ya maisha na kuishi.

Uzima, kusudi na haki ya maisha na kuishi. katika fremukazi ya Uono na Ufikirifu Mifumo, Trizaniumu, ndiyo hukadirisha ‘Sovereini Jumuifu’. Kwa mintarafu ya muktadha akilifu wa hayo yote, midenge minane ya gurudumu la Dhamma yajakufanyika ‘mapana ya nguvu ya pumzi ya uzima’ yapatayo kumi na mawili (12). Basi ndivyo kwamba, KUBU ina asili ya Mapana-Marefu-Kima-Kina yapatayo kumi na mawili (12); Dhahiri ni fumbo la ‘Pumzi’ ambavyo kitovu cha Yantra Dhamma huwakilisha ‘unje-Ndani’ wa yote na kila kitu—Mhimili wa 13 wa ‘Mchakato wa Mageuzi’ ulio ndiyo asili hasa ya ‘KUTOKA’ na ‘SALA’ katika ‘Mti wa Uzima’--Metafo ya ‘Bodhi’, mti aegemeao Buddha katika Utaamuliko wake, kwenye Bustani ya Mbawala.

Mhimili wa 13 wa ‘Mchakato wa Mageuzi’ ulio ndiyo asili hasa ya ‘KUTOKA’ na ‘SALA’ ilivyo ni asili ya hadhi/daraja la uweza wa ‘Upepo wa Mageuzi’, [Yabisi Platonifu ya Oktahedrani—Unje ndani wa KUBU](#) na hali mageuzi kamili, ni ‘Ukwantumumu wa Nuru ya Ufahamu’ katika ‘maji ya Uzima’ wote. Kwa mintarafu ya haya, ‘Platonifu Oktahedrani’ ina uwiliwili na ‘Platonifu KUBU’, na ‘Platonifu Ikosahedrani’ ina uwiliwili na ‘Platonifu Dodekahedrani’; Platonifu Tetrahedrani ina uwili uwili na namna yake tena yenyewe katika muakisikiko maingiliano. Basi ndivyo yawa, Tetrahedrani, katika ‘mapana na marefu-2D’ ya vina vya tafsiri ya uonekano, hukaidirisha picha sura ya ‘Nyota ya Daudi’.

‘Nyota ya Daudi’ ndiyo asili ya Mbingu na Nchi katika ‘Upatanisho’; Mukstadha akilifu wa ‘Uzima wa Yote’ ni fumbo la imani la ‘Tetrahedrani’ ya ‘Uweza, Nguvu na Utukufu’--uweza, nguvu na utukufu wa ‘Nuru ya Ufahamu’.

Tetrahedrani katika KUBU ndiyo asili ya ‘Midenge Minane’ ya ‘Gurudumu Dhamma’ kupitia Oktahedrani ya ‘Upepo wa Mageuzi’. Tetrahedrani ni ‘Moto’ wa ‘Dhamiri, Utendaji na Utukufu’ ;kwa hivyo hakuna mabadiliko/mageuzi pasipo ‘Moto’.

Dhamiri na Utendaji ndivyo asili ya ‘uweza na nguvu’ katika ‘nafsi’ ama ‘Kujiwazia nafsi/UTU’.

Tetrahedrani ndiyo ‘Jua la Maarifa’ kwa ajili ya Ku-JUA na kuto-KU-JUA katika ‘Pia ya UTU’--Ukonifu wa Dhahiri ya UTU kuwa ‘Nafsi’ katika ‘Madhahirisho’.

Ku-JUA na kuto-KU-JUA katika ‘Pia ya UTU’ ndiyo hasa asili ya ‘Dhukka’--utostabali wa ‘Uono kamili/Sahihi wa Mambo’ katika maisha. Ndivyo basi, dhukka hutafsirika kama ‘tabu/masumbuko/raha na karaha’ ya gurudumu linalotembea ‘kweche kweche’ kwa huwa kitovu chake hakijakadirika ukati kati hasa wa ‘Stamina’ na ‘Stabali’ wa kumudu kulibeba gari la ‘safari ya fahari za Maisha’ na ‘Kuishi’.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=ijuYCVMQuVw>

=====

### **Msafiri Kafiri: Mwenda Tezi na Omo...**

‘Nuru ya Ufahamu’ katika ‘Kujiwazia UTU’ huwa na ‘utenge wa kusudi’ katika mapana ya ‘makusudi ya Uzima wote’--Uzima na Uweza na Utukufu wa Miili ya dhahiri ilivyo ni ‘Usupasha-Wakati’. Kwa mintarafu ya haya, dhahiri yoyote katika usupasha-wakati ni ‘madanganyiko’ ya ‘Kujichagulia’ kwa (1) Dhamiri, (2) Vina vya tafsiri, na (3) Uono na Ufikirifu Mifumo.

Uono na Ufikirifu Mifumo katika ‘madanganyiko’ na ‘Kujichagulia’, maya na samsara ya gari la safari ya fahari za maisha na kuishi ndivyo hufanya ‘umbali na wakati’ wa ‘kudumu’ kwa mashauri ya ‘Kujiwazia UTU’. Kwa mintarafu ya haya, ‘kujiwazia UTU’ ni ‘Ndoto/Njozi’ katika ‘Mbalamwezi’ ya ‘Utukufu wa Mbingu na Nyota’; ambamo huoteshwa ‘mbegu za uzima wa miili’ ya kujisahau/kujidanganya ili kusudi la ‘Pia ya UTU’ ipate kudhihiri ‘Uweza, Nguvu na Utukufu’ wa ‘Kusafiri na KUTOKA’. Basi ndivyo yawa, gari na safari ndiyo mambo kutwaa miili na karma katika ‘Utukufu wa Mbingu/Nchi na Nyota’.

‘Umbali na wakati’ wa ‘kudumu’ kwa mashauri ya ‘Kujiwazia UTU’ katika ‘dhukka’, kiuono na ufikirifu mifumo, ndiyo muktadha akilifu wa (1) Matendo, (2) Wakati na (3) Matukio. Kwa mintarafu ya hili, kujiwazia UTU ni kupanda mbegu ya ‘matendo, wakati na matukio’ ilivyo ni muktadha wa ‘Kujichagulia’--ufanyaji maamuzi na kuchagua mapito kwa wakati. Basi ndivyo yawa, kupanga ni kuchagua na akipandacho mtu ndivyo, katika kupita kwa kipindi cha wakati, atavuna kwa kadiri ya kusudi na matendo yake; hauwezi kupanda pilipili ukavakuvuna parachichi... ‘Dhukka’ ni matokeo ya yote matatu (1) Ujinga/Kutofahamu, (2) Kutofahamu mambo ilivyobora, na (3) Makusudi yenye kuharibika... Mapelekeo ya ‘Nia ya UTU’ katika uhasimu wa Kujua na Kutokujua ilivyobora.

Buddha alifundisha habari za ‘[Marga](#)’ ilivyo ni Miongozo ya Wongofu kwa ajili ya Kumalizana na ‘Dhukka’-- Dhukka na muambatano wake wa ‘Samsara’ na ‘Maya’. Kwa mintarafu ya hili, miongozo hii yaja kuwa [Gurudumu la Midenge Minane la Buddha Mkuu](#); na tena Muktadha Akilifu wa [Dhammapada](#)—Njia ya Buddha.

Miongozo/Mafundisho ya Wongofu ya Buddha, kiuono na ufikirifu mifumo, ni ufunguo khasa wa ‘Uono na Ufikirifu Mifumo’. Kwa mintarafu ya hili, Njia ya Buddha ni ‘Usahihi wa katikati wa (1) Dhamira, (2) Mawazo/Kujiwazia UTU na (3) Uono’ ambavyo mifumo ya kuishi/maisha hukadirisha (1) ‘utabia binafsi’, na tena (2) ‘utabia wa kishirika’ kwa ajili ya (3) ‘Mazingira Rafiki’ ya ustawi wa wote wenye ‘Nuru ya Ufahamu’, miili ya uweza na Kuchagua/kujichagulia ilivyobora. Basi ndivyo yawa, kwa kheri ya Dhammapada ‘Mawazo/Kujiwazia UTU’ ni kitovu cha mhimili wa imani ambavyo ‘Nuru ya Ufahamu’ ni ufunguo wa wongofu—ufunuo wenye kupitiliza mashauri ya ‘vina vya tafsiri’ na ‘dhamira’ ilivyo ni moja kwa moja.

Haya ni mambo ya akili na uakilifu.

Akili na uakilifu ni 'Umodulishi wa Ufahamu'; na ufahamu, wenyewe ni 'Nishati Nukta Sifuri'--nishati nukta sifuri ya vyote na kila kitu.

Uelewa huu ni wenye kushiriki uwanja na marefukio yale yale ya mashauri ya 'maya'-- viini macho vya sura ya vitu/mambo vyenye asili itokanayo na 'fremu ya Uhalisia wa Muona na Mkazo macho wake.

Ni kutokana na muktadha huu wa Uhalisia wa Muona na Mkazo wake macho, Gautama Buddha alijenga msingi wa Kweli nne(4) za tunu kuwa kwamba ndiyo mwanzo wa yote ya Kujichagulia ili kuja kuwa huru na 'Samsara ya Maisha yenye Mauti'.

Kwa mintarafu ya haya, 'Samsara', utwaaji mwili wa nyama wa mwenyekuwa sentienti hufuatisha (1)'Maua-Sura Akilifu' ya (2)'usababishano wa maadili ya ujuzi wa jema ama/na baya' na tena kuambatana na (3)'mafikara/misukumo ya hisia kwa ajili ya raha ama karaha/matakwa ya moyo/matamano ya kiutu'.

Ipo asili ya ndani hasa ya hulka za kitabia kwa ajili ya 'Kutangatanga kwa nafsi-roho' na hali hapo hapo upo uhalisia usiobadilishika milele--wa kudiriki kusemwa kana ule uliombali kupitiliza uweza wa akili kufaa kutumika kiuakilifu. Mbali kupitiliza 'uweza akilifu' huelezwa na wasikirifu kama 'UKIMYA'.

Buddha alishughulika kwa ajili ya mawezekano ya mwisho kabisa ya mtu mmoja kuweza kufikia kupata hali ya kuwa fahamu na ULE UKIMYA. Hali ambayo hakuna nafsi/nafsi-roho, na tena basi 'hakuna Wakati'.

Buddha aliita njia ya kusharabika kwenye hali hii ya Ukimya, njia kuelekea Sammadhi katika UTU pekee, kuwa ni 'Dhammapada'. Ndivyo basi, katika mwelekeo wa Dhammapada ni uhalisia wa 'Gurudumu la Dhamma'--lililoitwa na Buddha, njia ya Manane yajayo na kusudi moja la wongofu.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=iw65evLgQgc>

=====

### **Marejeo Ngamani: Kujisukanya na kujikung'uta mavumbi**

Njia ya Manane yajayo na kusudi moja la wongofu, na dhamma yake katika UTU pekee, ndiyo yenye baraka ya kukadirisha 'Sovereini Jumuiifu'; na basi zaidi 'Trizaniamu'. Samma/ Usahihi wa (1) Uelewa : Ditti, (2) Dhamira : Sankappa, (3) Kauli : Vacha, (4) Kitendo : Kammantha, (5) Uisho : Ajeeva, (6) Jitihada : Vayama, (7) Uakilifu : Sathi, na (8) Umbonishaji fahamu : Samadhi.

Maana mfanano kwa 'Usahihi/Samma' ni 'Mizania'; kwa mintarafu ya hivi ni mizania ya 'hisia ufahamu' na 'vina vya tafsiri za urazini' zinazotupatia mkononi mikutadha 'Kujifahamu' yenye baraka bora kwa wakati--aina ya 'kujifahamu' kwenye mzizi iliyojichomeka katika 'Uakilifu' na 'Uisho'. Mikutadha ya Uakilifu inatumikika kwenye 'Uelewa', 'Kauli' na 'Kitendo'; kwa maisha ya kila siku na

vivyo hivyo panapo mmoja na mwingine wanavyoshiriki makutaniko ya shughuli; na wakati huo huo hutumikika vivyo hivyo kwenye 'Dhamira, Hekima na Uisho' kama maegamio kwa 'Uono Mifumo' kwa ajili ya 'maisha yasiyo na mapambano/manyukano' na uwepo wote wa vitu.

Mikutadha ya Uakilifu unatumikika kwenye 'Jitihada', 'Dhamira' na 'Umbonishaji fahamu' kwa ajili ya 'kumodulishia juu ama chini' hisia fahamu za uhalisia wa kifiziki sambamba na sehemu zake uhesabu ilivyo ni 'fikra na hisia'. Kwa mintarafu ya hili, 'Uzimishaji wa Akili' ni hali bahatifu iliyo huru na 'Mawazio ya Maisha'.

Mikutadha ya Uakilifu ni Vipassana--Michakato ya Uonefu/Ushuhudiaji wa fahamu pasipo 'kujitambulisha na yatokeayo'. Kwa mintarafu ya hili, vipassana ni mbinu mahsusi ya kiufundi ya kuitafuta nukta sifuri ya akili ambapo ufahamu pasi umodulishi waweza 'kuishika' pasipo 'unafsi kupata jina'-- mapelekeo ya maana ya 'Utupu' katika 'Utu Mmoja'.

Kwa mabaki ya asili-akili yenye uingiliano wa chini kabisa kivitendo na mambo, kuelekea hali ya 'Utupu' kabisa kabisa, ilivyo hali ya mapito ya kuliishi jambo kwa mwenye ushuhudiaji/uonefu, mtu wa vipassana katika samadhi hughubikwa na (1) hisia za juu za furaha ya moyo, (2) amani ya moyo, na (3) kina kisichofikika mwisho cha 'Amani ya Utu'.

Kwa mabaki ya asili-akili yenye uingiliano wenye ukuu wa kivitendo na mambo, kwa mtu wa vipassana katika samadhi, mapana yasiyokifani ya (1) ulimwengu/alimwengu, (2) mifanyiko akilifu na (3) ufanusi wa mambo; hufanyika 'kuwezekana kufahamika' kama mapitio ya moja kwa moja ya uzoefu wa mambo katika umbonishaji

akilifu wa fahamu kwenye '[madanganyifu ya nafsi/Ukuwa na Wakati](#)'.

Kwa mabaki ya asili-akili yenye uingiliano kivitendo na mambo wenye ukuu, gurudumu la dhamma linaweza kufanyizwa ukuu kutokea upande pitilizi wa uhalisia wa maisha ili kuwezesha (1) 'Umasiha/Mahdi/Manyoosheko udhahiri-nafsi wa Boddhisatva/Ukuwa UTU' na (2)'wakati'. Uhalisia ulionyookea mbali kupiliza kawaida ya mambo, katika mapokeo ya Kibuddha, ndivyo basi 'kinu cha mzigo-msalaba' wa katikati wa miduara ya gurudumu la maarifa kwa Buddha, mtu wa utaamuliko, aliyefanyika/anayefanyika 'Mkuu'.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=ZaYMzvjsrjQ>

=====

### **Kila Mtu anauchukua Mzigo wake yeye Mwenyewe**

Msalaba ilivyo ni ukadinali wa (1) Uelewa, (2) Kauli, (3) Uisho, na (4) Uakilifu;

Kuwa basi:-

(1) Kauli na Uisho ndiyo huleta muktadha wa 'Shika Neno, Tenda Neno' na

(2) Uelewa na Uakilifu ndiyo asili ya Vipassana na Samadhi kwa ajili ya kukadirishia 'Mbawa-UTU za kujichagulia' ambavyo ni muktadha wa 'Dhamira' katika 'Umbonishaji wa fahamu' ili kuakisi 'Jitihada' na 'Kitendo'.

Kwa mintarafu ya haya, kulizingurusha gurudumu la dhamma ni jambo bahati lijalo kwa fasaha za (1) Kuhama sura moja hata ingine ya kujichagulia utukufu, (2) Ku(ji)nyooshea miongozo ya mageuzi ya sura na utukufu, na (3) Kusogeza mahalisia ya ujumuifu wa ufahamu ilivyo ni mafungamano ya nafsi-akili-maumbile ya sura.

Kila mmoja wa kiumbe awe na fahamu ama asiwe na fahamu anatendesha dhamma yake mwenyewe, uhalisia ulionyookea mbali wa (1) Karma, (2) Akili, na (3) Madhamirio--KUBU za 'Supasha-wakati'/'Nafsi/Akili. Alamu zingine za Ukuwa Kiumbe na Asili wakati wote huwepo kama manyookeo hai ya mafikara, hisia na madhamirio -- vyenye mambo ya ushirika kwa mapelekeo ya 'kulizungurusha gurudumu la dhamma'; kubahatisha ujio wa asili za (1)'Tripitaka' na tena kwa mujibu wa (2)'Triptika' katika (3)'mapana ya Trikaya'. Kwa mintarafu ya haya, uisho sahihi--samma Ajiiva, ni ufunguo wa 'Kuhama sura moja hata ingine ya kujichagulia utukufu' kulingana na hamasa ya kiutu katika Nafsi/Ukuwa Kiumbe na tena wakati.

Miditisha ni muhimu hasa kwa ajili ya Dhammapada -- utimilisho wa matakwa tunu ili kuja kuwa Buddha anayeishi; na hii ni njia upweke, ya mtu mmoja kipekee yake na tena uhuru wake. 'Kuabudu' na 'Kujitoa moyo' kwa 'chenye kheri' si miditisha -- haya ni mengine ya 'mapokeo ya kukamilishana'; na basi wakati mmoja haya yaja kukutana/kuingiliana na mielekeo kwa ajili ya 'Maisha yanayoizidia juu Kawaida'

Mbinu-kazi ya Buddha kwa ajili ya 'Nidhamu ya Kiakili', ilivyo katika njia ya Buddha, na tena kwa ajili ya kufikia utaamuliko ni 'Via Negativa'. Kwa mintarafu ya hili, mwenye kufikia utaamuliko

anakwenda kuikosa ladha ya kigulu na njia kupitia tuseme 'kujitoa moyo/Upendo/Huruma'; ingawaje mielekeo yote miwili, miditisha na mapendo, huishia kwenye kilele cha 'Utaamuliko Mmoja wenye kujumuisha yote'. Kwa hivyo ndivyo kusema asili ya 'ufahamu-nafsi-akili-maumbile sura' hufanya kuinuka kwa 'mikutadha akilifu yenye kukamilishana' ya ukweli wa YOTE.

=====

[https://www.youtube.com/watch?v=vj6GM-C5vks&list=OLAK5uy\\_kod3C57m3iJKirqXygSz4ciODbXN6RmBE&index=1](https://www.youtube.com/watch?v=vj6GM-C5vks&list=OLAK5uy_kod3C57m3iJKirqXygSz4ciODbXN6RmBE&index=1)

=====

### **Isemwavyo 'Nira iliyo ni Nyepesi'**

SASA, haya yanakujaje na 'Utaifa' wa Tanzania—kwa mfano?

Kiufundi, 'Utaamuliko jamii' ni ufunguo wa 'Ulinzi' na 'Kazi'--Ulinzi na kazi kwa ajili ya kulijenga taifa, kuujenga UTU.

UHURU, UDUGU, HAKI na AMANI ni KISU ilivyo ni ALMASI ya UBUDDHA; Maisha na Uisho ni 'Mchezo wa Mapiku' ambavyo 'Masumbuko na Tabu' ni matokeo ya Kuzichanga karata kichaa za Uzima wa Miili.

Kwa hivyo kama ilivyo dhahiri shahiri katika Yantra Dhamma, Gurudumu la Dhamma huja na Duara nne (4) na Mraba wa Maisha. Duara katika kila upande wa Mstari wa Mraba wa maisha ni uashirifu wa 'Usahihi wa Vitovu' vinne ya Tunu ya Utu kama alivyofundisha Buddha Mkuu.

Kama alivyofundisha Buddha, kukosa fasaha ya vitovu vya uono na tafsiri ya mambo ndiyo adha kuu ya Maisha na Kuishi -- kukadirisha Kweli Nne (4) zilizo ni TUNU.

Kila ‘Pembetatu’ inayokabiliana na upande wa Mraba ni ‘Vekta Dhamiri’ ya UTU na Maadili—Thrishiksha. Kiufundi, pembetatu ya muktadha wa vekta dhamiri ndiyo asili ya pembetatu ndani ya duara katika alama oanifu za Trizaniumu.

Basi ndiyo yaja kuwa mifumo yote ni asili ya pembetatu za vekta dhamiri kujimizanisha katika mapana na marefu ya ‘Mraba wa Maisha’—KUBU za ‘Supasha-wakati’/‘Nafsi/Akili’. Alama ya ‘Mifumo’ katika Trizaniumu ndivyo basi khasa pembetatu mbili zinazokinzana uelekeo huku zikishiriki kitovu cha nguvu na uweza katika ‘mstari wa mizania’. Duara yenye Kitovu chenye kushiriki kitovu za mstari wa mizania ni asili ya ‘Mboni ya Fahamu’.

‘Mboni ya Ufahamu’ katika vitovu vya (1) vitendo, (2) dhamira na (3) jitihada ndiyo khasa asili ya ‘Uelewa’ na ‘Uakilifu’ ilivyo basi ni asili ya ‘Vipassana’ na ‘Samadhi’ kwa ajili ya kukadirishia ‘Mbawa-UTU za kujichagulia’.

Mintarafu ya haya ndiyo yanakarisha ingilio kwa ‘Hekima, Umoja na Amani’.

Msalaba ilivyo ni ukadinali wa (1) Uelewa, (2) Kauli, (3) Uisho, na (4) Uakilifu; Katika taifa la Tanzania ndiyo kiini cha ‘kunena na kutenda’ kwa ajili ya udhamirifu wa UHURU, UDUGU, HAKI na AMANI.

Kiufundi HEKIMA na AMANI huja na Utangamano wa (1) Jitihada katika muktadha wa usahihi wa katikati wa (2)Dhamira na (3) Matendo; Ambavyo ‘UMOJA’ ni koherensia ya nidhamu ya vitendo kulingana na ‘Miongozo’--Mraba wa Maisha katika Yantra Dhamma ndiyo ‘Muakisiko’ wa ‘Vitendo vyenye miongozo ya UTU bora’, Dhamma.

Koherensia ya nidhamu ya vitendo kulingana na ‘Miongozo’ ndiyo msingi wa Taifa na Ontolojia ya Utaasisi wake wa Dola na Mamlaka ya wananchi. Kwa mintarafu ya hili, katiba ni ‘Mkusanyiko wa Miongozo’ kwa ajili ya ‘Ontolojia ya Taasisi’ na ‘Usivilai wa Wananchi’. Fanusi ya ‘Utaamuliko Jamii’ ndiyo msingi wa Ku-Jua na Kuto-Ku-Jua kunakokadirisha Haki na Wajibu wa ‘Wenyanchi/Wananchi’ kwa kuwa ufahamu wa UTU na UZALENDO ndiyo hujenga ubayanifu wa Kujichagulia katika ‘Kheri’ ama ‘Mikosi’ ya UTAIFA.

Kwa hivyo ufundi wa Katiba ni kujenga ‘miongozo’ kwa mambo ya Kiroho, Maadili na Miiko; si michoro ya ‘Sura na mipango’ kwa ajili ya sura na nchi tawala kwa ‘vina vya kimasahafu’ ya miundo na utaasisi ‘iliyokubuhu’ maelezo na uchanganuzi wa ‘taasisi ndani ya taasisi’. ‘Miongozo’ kuwa ‘Sheria Mama’ ni ingilio la ‘taratibu na kawaida’ za kijamii—basi si ‘ufunguo wa ufahamu’ khasa. ‘Utaamuliko Jamii’ ndiyo hasa ‘Ufunguo wa Ufahamu’ na ndiyo ‘Dume la Shupaza’ la ‘Maisha na Uisho’...

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=T9UtTXu9pZo>

=====

## **Mambo ya Mlimani: Muongozo kwa ajili ya Taamuli, Kazi na Ulinzi**

Katika ujenzi wa taifa la Tanzania na tena Afrika Mpya, 'Mwenge wa Uhuru' kuwekwa juu ya Mlima Kilimanjaro ndiyo 'ufunguo wa ufahamu' kwa ajili ya 'Uono na Ufikirifu Mifumo' juu ya 'Uelewa'-- Uelewa unaopaswa kuwa kwa 'wananchi wote' ili Hekima, Umoja na Amani vidhihiri utukufu wa sura na kheri ya taifa la watu.

Katika Gurudumu la Midenge minane la Dhamma, 'Uelewa' ni ncha moja ya ukadinali, KASKAZINI, inayosimama katikati ya mdenge 'Umbonishaji Fahamu/Samadhi' upande wa kushoto; na mdenge 'Dhamiri/Sankappa' kwa upande wa kulia. Basi ndiyo kuwa, mizania ya mapana ya kujichagulia katika sura ya nchi na tawala huja na yale yahusiayo miongozo mahususi ya 'Udugu na Haki' ili kuzaa 'UJAZI' na 'LIBERTI'.

Katika Katiba ya JMT miongozo hii mahususi ndiyo hasa yale yaliyotajwa dhahiri kama:-

- 'Maendeleo ya uchumi wa Taifa yanakuzwa na kupangwa kwa ulinganifu na kwa pamoja';
- 'Kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi, na kazi maana yake ni shughuli yoyote ya halali inayompatia mtu riziki yake';
- 'Aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, uonevu au upendeleo zinaondolewa nchini';

- 'Matumizi ya utajiri wa Taifa yanatilia mkazo maendeleo ya wananchi na hasa zaidi yanaelekezwa kwenye jitihada ya kuondosha umaskini, ujinga na maradhi';
- 'Shughuli za uchumi haziendeshwi kwa njia zinaweza kusababisha ulimbikizaji wa mali au njia kuu za uchumi katika mamlaka ya watu wachache binafsi';
- Nchi inatawaliwa kwa kufuata misingi ya DEMOKRASIA na UJAMAA.

Miongozo hii, kwa mfano, ndiyo hasa '[Gongo kwa Msafiri](#)'--Taifa la Tanzania ni Msafiri katika 'Uelewa' na 'Uisho' wa Maisha, KASKAZINI na KUSINI ya Gurudumu la Dhamma; Ambavyo (1) 'Umbonishaji wa fahamu upo kwenye shauri la Maendeleo ya Uchumi wa Taifa'; (2) 'Vitendo ni Kazi' kwa ajili ya Riziki—Ujenzi wa Taifa ni shughuli ya 'chakula, mavazi na malazi'; (3) Uakilifu wa 'Usalama wa Raia na Mali zao' ni jambo liendalo sambamba na 'Uaminifu wa Mifumo' na 'Utaasisi' katika 'kheri ya usivilai na ustawi' wa 'wenyenchi'--wananchi wote ndiyo wenyenchi katika 'Utaamuliko Jamii'.

Hili la 'Utaasisi' katika 'Kheri ya Usivilai na ustawi' wa 'wenyenchi' ndilo hukadirisha Utaasisi wa jeshi la ulinzi wa raia na mali zao kuja kuwa na alama za moja kwa moja za (a) 'taji la muktadha mwenge wa Uhuru', (b) zana za jadi kwa kazi na ulinzi na tena (c) kaulimbiu ya 'Shika Neno, Tenda Neno: Usalama wa Raia'.

Kuhusu Matumizi ya Utajiri wa Taifa (4) ndiyo 'ukumbusho' wa 'dhamiri ya UMOJA' kuwa na mazingatio ya kushiriki muktadha wa maendeleo ya wananchi kwa mihimili ya ukwamuzi wa 'dhukka'--msingi hasa wa shughuli za serikali ya wananchi ni huduma za jamii kama upatikanaji wa Elimu, Huduma za Afya, Miundo mbinu ya

Uchukuzi na ‘Starehe’ za jamii. Kwa mintarafu ya haya, sera na sheria za nchi ni shurti ama/na taratibu kwa ajili ya mahitaji ya usivilai na utamaduni.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=wVxMopianEc>

=====

### **Fimbo ya Musa: Miongozo kwa ajili ya ‘Udugu’ na ‘Haki’**

Shughuli za uchumi kutoendeshwa kwa namna ama/na njia za kuweza kusababisha ulimbikizaji wa mali ama njia kuu za uchumi katika mamlaka ya watu wachache binafsi (5) ni ‘Shauri Dume la Shupaza’ la ‘haki na fursa sawa kwa wote’; japo hili kiufundi ndiyo ‘mtihani’ wa ‘UTU na Matamanio Batili’ katika ‘Uelewa’. Hivyo basi, hili ndilo hasa linalolazimu ‘Hekima ya Buddha’ juu ya ‘TUNU Nne za UTU bora’ iwe kitovu cha ‘Utaamuliko Jamii’ ili Umma wenyewe ujenge ‘kinga’ na ‘imani’ ya utu bora—si kupotoka na mambo ya utaasisi wa ‘sera na sheria’ za nchi zisizoendanana na ‘Nuru ya Ufahamu’ iliyoko katika jamii kumbaizi.

Kuhusu nchi kutawaliwa kwa kufuata misingi ya DEMOKRASIA na UJAMAA (6); hili ni shauri juu ya kheri ya ‘uhuru wa kujichagulia’ na ‘Ujamii uliotaamulika’ katika misingi ya Tunu Nne, UHURU-UDUGU-HAKI-AMANI; Kiufundi, jamii isiyo na ‘Uono na Ufikirifu Mifumo’ katika ‘upeo’ na ‘uwezo’ wa uakilifu wake, yawa haina ‘Kinga ya Madhalimu’ wala ‘Nishani za Utu Bora’. Shurti ya ‘Sera na Sheria’ vyaweza kuja na vimvuli vya mwangaza na ni si ‘Nuru ya Ufahamu’. ‘Mwenge wa Uhuru’ ni karata ‘Dume la Shupaza’ kwa ajili ya DEMOKRASIA na UJAMAA.

Miongozo hii sita (6) ya mfano, ndiyo hasa ‘[Gongo kwa Msafiri](#)’-- Taifa la Tanzania ni Msafiri katika ‘Uelewa’ na ‘Uisho’ wa Maisha, KASKAZINI na KUSINI ya Gurudumu la Dhamma; ambavyo ‘[karata Dume la Shupaza/Jembe](#)’ ni mhimili mmoja na ‘[karata Dume la Kisu/Almasi](#)’. Haya mawili ndiyo ‘huungamisha fahari za Mbingu na Nchi’ katika UTU na UZALENDO. Utamaduni wa taifa ni jumla ya mambo ya mbingu na nchi ambavyo usivilai ni ulali wa msalaba wa ukadinali, na tena MAGHARIBI na MASHARIKI ya gurudumu la dhamma.

Magharibi na Mashariki ilivyo ni ‘Kulia’ na ‘Kushoto’ ya pahala pa ‘Utakatifu wa Sura ya Nchi na Tawala--Utakatifu katika Kazi na Sala’ ndipo kwenye ‘USHIRIKA WA KUJISIKIA’, Magharibi, na ‘UJAMAA / SOVEREINI JUMUIFU’, Mashariki. Kwa mintarafu ya haya, Maisha na Uisho huandamwa na ‘Nuru ya Ufahamu’ ama ‘Mbalamwezi ya Vimvuli ya Tafsiri ya mambo’ katika UTU na Nafsi. Ikiwa kushoto ni ‘[Dume la Mavi ya Mbuzi](#)’ basi kulia ni ‘[Dume la Kopa](#)’.

Alama ya Karata ya Magharibi na ya Mashariki ndivyo basi viwili ambavyo huakisi ‘tambarare ya nchi’ kwa ‘hisia/mapenzi mema/mwendano wa fahamu katika mshikamano ama misugvano’. Ndivyo basi mambo ya nchi, jamii na tawala hutiwa alama za utaasisi na uhai kwenye sanaa za Nembo na Bendera za jumuiya/jamii/nchi-taifa/dola—[Alama za mategemeo na Upepo wa Uchukuzi wa fahamu za wanajamii kama kikundi kimoja cha watu](#).

Mambo ya mkono wa kulia na kushoto ndiyo huyakinisha jitihada, dhamira na mustakali wa ‘kuwa’ ama ‘kuja kuwa’ kiutu, muundo na matendo—mambo ya NIA na UAKILIFU kwa jinsi ya yote mawili: (1) hisia na (2) mawazo. Kwa hivyo muundo na uweza wa

kimatendo ni mambo yenye asili ya ‘fizikia’ na ‘metafizikia’ kupitia ‘NIA’. Ndivyo basi ‘NIA’ ni ‘[Gongo kwa Msafiri](https://www.youtube.com/watch?v=5MIuCQnEA6c)’ kwa mambo ya nchi na pia mbingu... Mambo ya ‘Msalaba’ wa mtu katika SUPASHA-WAKATI. Muakisiko wa Nia katika vitendo ni kazi na utu ardhini, vivyo hivyo ‘Mbawa’ kwa ajili ya ‘uwepo’ na ‘wepesi kwenye kushida mapana na marefu ya nchi’.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=5MIuCQnEA6c>

=====

### **Alama za Uchungaji: Muongozo wa Ulinzi na Malango ya UTU na Ustawi katika Kujichagulia**

Mambo ya ‘Kazi’ na ‘Mbawa’ ndiyo huja kwa alama za ‘zana za kazi’ katika nembo za nchi-taifa/dola; ni kukaa kwake kama mkasi ‘X’ ndiyo topografu wazo kwa metafo ya ‘MBAWA’--mawezekano ya kupaa juu na kushinda ‘mapana na marefu ya nchi’ na amali zake. Basi ndiyo alama ya ‘X’, katika Trizaniumu, huwakilisha uwezekano wa kufanyika kwa ‘NIA’ katika UTU ambavyo msalaba hupambanua ‘nasibu’ ya ‘JAALA’(OX-OY)--Kujichagulia.

Kwa nchi ya Tanzania, NIA huja na ualama wa ‘SHOKA na NYENGO’; kwa kutumia Uono na Ufikirifu Mifumo, viwili hivi ndivyo hukadirisha ‘NIA’ ilivyo ‘KAZI na KUPAA JUU’ – kupasua USUPASHA-WAKATI. NIA ni muktadha akilifu wa ‘SHIKA NENO, TENDA NENO’ kwa hivyo ni khasa pembe tatu ya Vekta za Udhamirifu wa jambo/mambo—kwenye Trizaniumu, zinazobayanisha ufraktali wa triadi za (1) UONO, (2) ONTOLOJIA YA TAASISI, na (3) SURA NA MIENENDO YA JAMII.

Kwa nchi ya Tanzania, NIA huja na ualama wa ‘SHOKA na NYENGO’; kwa kutumia Uono na Ufikirifu Mifumo, viwili hivi ndivyo hukadirisha ‘NIA’ ilivyo ‘KAZI na KUPAA JUU’ – kupasua USUPASHA-WAKATI. NIA ndiyo muktadha wa fizikia na metafikia ya UTU katika YANTRA DHAMMA ambavyo Nyoka Wawili wanajisokotea kwenye Uhimilili ilivyo ni ‘[Gongo kwa Msafiri](#)’ ili kupaa na kutanuka katika mbingu... Basi ndivyo yawa alama ya ‘NIA’ kwenye Trizaniamu hujakukadirisha MRABA ALMASI wa UTU kwenye kuegemeana na ‘MRABA DHAMMA’ wa UTU. Dunia, Maisha na Uisho ni kusudi la mafumbo ya ufahamu, kujiwazia UTU na MATUKIO ambavyo Machaguo ya Kitaasisi yanakadirisha yote mawili: (1) Werevu wa Nyoka, na (2) UTU kupata MBAWA kwa ‘NISHANI ya UTU BORA’.

Werevu wa ‘Nyoka wa UONO’, kiuono na ufikirifu mifumo, ni muktadha akilifu wa yote mawili (1) ‘kula kwa jasho’ pale ambapo ‘Hakuna Paradiso’--’Ulimwengu wa Shetani/Ibilisi, madanganyiko ya KIUTU’ kuja kwa Samsara na Maya, na tena basi, (2) Uono fasaha wa ‘Samsara’ na ‘Maya’ kupitikia ukadinali wa UELEWA SAHIHI-UISHO SAHIHI-UAKILIFU SAHIHI-KAULI SAHIHI, Basi ndivyo yawa, KAULI SAHIHI ni ufunguo wa ‘SHIKA NENO, TENDA NENO’ ambavyo MRABA DHAMMA hutanuka sambamba na MRABA ALMASI kwa vekta udhamirifu zipatazo ‘33’. Hivyo basi, kiufundi, vekta udhamirifu zipatazo 32 kwenye MRABA DHAMMA hukamilishana na vekta dhamirifu zipatazo 12 katika MRABA ALMASI kuikadirisha ‘NYOTA YA DAUDI’--kitovu cha ‘13’ na ‘33’ za YANTRA DHAMMA.

Vekta Udhamirifu ndiyo asili hasa ya ‘MIFUMO’ na basi ‘UONO NA UFIKIRIFU MIFUMO’ kwa kuwa MAISHA na UISHO ni fumbo la imani kwa ‘Nuru na Giza’ katika FANUSI UTU. Basi ndivyo ‘NYOTA YA DAUDI’ huleta KUBU ya ‘Matriksi Uzima wa Miili’. Tena zaidi,

KUBU ina ufunguo wa ‘fizikia’ na ‘metafizikia’ ya ‘UTU na KUJICHAGULIA’ ambavyo ‘mauti’ ama ‘Uzima wa Milele’ huyakinisha USHINDI kupitiliza ‘Samsara’ na ‘Maya’.

Kitovu cha ‘13’ na ‘33’ kwa misukumano ‘ndani nje’ ya uvekta dhamirifu katika YANTRA DHAMMA ndiyo asili ya ‘uweza, nguvu na utukufu’ wa ufanyayo yote na kila kitu—kwa mambo yenye kuonekana na hata pia yasiyoonekana. Basi ndiyo yawa, Duara la Tano katika Yantra Dhamma ndiyo ukadirifu wa ‘[SHEKINAH](#)I’ katika ‘maarifa ya kimalaika’; mahala pa UWEPO, NGUVU na UTUKUFU, unaofutika mbingu na nchi zote ilivyo ni ‘utimilifu wa dahali’--USUPASHA-WAKATI.

‘[SHEKINAH](#)I’ hushikilia yote na vyote ilivyo ni ontolojia ya ‘Mbingu na Nchi’--katika mapana ya uelewa wa kileo, 2024, ndivyo kusema: mapana ya fahari za nyota, sayari na makundi ya nyota katika utupu usiokuwa na mwanzo wala mwisho wa ‘Utimilifu wa Dahali’. Basi ndiyo yawa, [SHEKINAH](#)I ndicho kitovu hasa cha ‘MUONA ni MUONWA’ ambavyo ‘uzima ya miili’ yenye ‘ufahamu na kujitambua’ hujibaini ‘HAKIKA’ wa kheri zake katika kimo-mapana-marefu-kina ilivyo ni ‘KUBU za MADHAHIRIKO’. Basi ndiyo tena, YANTRA DHAMMA ni LUGHA ya Utukufu wa Miili na Madhahiri ilivyo ni MAGEUZI yasiyo na mwanzo wala mwisho bali mifumo ya vekta udhamirifu katika (1) UELEWA, (2) KAULI, (3) UISHO, na (4) UAKILIFU.

YANTRA DHAMMA ni LUGHA ya Utukufu wa Miili na Madhahiri ilivyo ni MAGEUZI yasiyo na mwanzo wala mwisho; ambavyo kwa Miongozo ya Mafundisho ya Buddha—Dhammapada UTU unaweza kujinasibu na ‘Kituo’ cha kupitiliza fahari zote za mbingu ama nchi kwa ‘UMBONISHAJI SAHIHI’ wa ‘UONO’--Samma Samadhi. Kwa

mintarafu ya hili, Umbonishaji Sahihi wa Uono ndiyo khasa asili ya ‘Ontolojia ya Taasisi’ kuwa na ualama wa ‘Duara na Nukta’. Katika YATRA DHAMMA jamii inayiishi Dhamma kwa NISHANI YA UTU BORA ndiyo hukadirisha (1) ‘Duara na Nukta’ upande wa Kaskazini—ualama wa Ontolojia ya Taasisi, (2) Vesika Paisisi ya utonalishi wa fahamu upande wa Magharibi—ualama wa ‘Kujisikia’, (3) Msalaba wa Maisha na Nia—ualama wa ‘Kujichagulia’, na (4) Gurudumu la Dhamma – hakika ya ‘Sovereini Jumuiifu’.

Asili ya ‘Ontolojia ya Taasisi’ ni (1) Kujisikia, (2) Miundo, na (3) Ushawishi amabvyo hukadirisha (1) Nia, (2) Matendo, na (3) Miongozo katika Maisha na Uisho. Kwa mintarafu ya haya ‘UONO’ ni jambo mtambuka kwa (1) JAALA, (2) KUMBUKUMBU-UZOEFU, na (3) MIFUMO. Basi ndiyo yawa, katika Trizaniumu (A) Jaala huwa ni ualama wa ‘Kimvuli’ cha ‘Kujichagulia’; (B) Kumbukumbu-Uzoefu huwa na ualama wa ‘Mapana wazi ya Mistari ya Nchi na Mbingu’; na (C) Mifumo huwa na ualama wa ‘Pemberatu Mbili katika Mizania ya Mapana ya Nchi’.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=ymxj9SSvgr8>

=====

### **Mifumo na ‘Mafumbo ya Imani’ : Kukadirisha Jithada za UTU na Nyakati**

Mifumo kuwa na ualama wa ‘Pemberatu Mbili kukabiliana kwa kadiri ya Mizania ya Mapana ya Nchi’ ndiyo ile asili khasa ya Midence Minne ya Buddha, ukiachia ukadinali wa Uelewa-Kauli-Uisho-Uakilifu; yaani hatma ya (1) Umbonishaji sahihi wa fahamu, (2) Dhamira Sahihi, (3) Vitendo Sahihi, na (4) Jitihada Sahihi. Basi ndiyo yawa, ‘umbonishaji sahihi’ ndiyo unayokadirisha ‘Ontolojia ya

Taasisi’ yenye kheri kwa ajili ya ‘dhamma ya jamii’ katika ‘Sovereini Jumuiifu’. Kwa mintarafu ya haya, ndivyo basi alama ya ‘UONO’ katika Trizaniumu ni ‘midenge minane ya Gurudumu la Dhamma katika kinvuli cha Ontolojia ya Taasisi’. Vivyo hivyo, mifumo ni muakisiko wa veka dhamirifu kwa kadiri ya ‘Nishani ya UTU Bora’ na ‘Nguvu ya KUBU kushikilia Matriksi’ yake. Mambo ya Nyakati, Matukio, ni matokeo ya Nishati ya UTU na udhamirifu wa matendo yaendanayo na muktadha wa kujiwazia utu—ikiwa ni kwa utaamuliko basi matukio huja na kadiri ya fahari ya sovereigni jumuiifu, ama sivyo huja kwa ‘Sura na Mienendo wa Jamii’ kwa kadiri ya ‘Utonalishi wa Fahamu, Miundo ya Utendaji na Utendaji wenyewe’ wa jamii...

Ualama wa ‘Pemberatu Mbili kukabiliana kwa kadiri ya Mizania ya Mapana ya Nchi’ ndiyo asili ya ‘mfumo’ ambavyo (1) UONO, na (2) UHAKIKA ni fumbo la ‘UWEPO’ na ‘UZIMA WOTE’--Uzima wa Milele. Kwa mintarafu ya haya mawili, MIONGOZO hutawala SURA na MAGEUZI na UTUKUFU wa yote na mote. Basi ndiyo yawa, katika MRABA ALMASI, nishati ya UTU BORA huja kwa mafumbo ya MUONA ni MUONWA ilivyo ni muktadha wa nguzo kumi na mbili (12) za ‘Imani’ na ‘Matendo’ kwa ‘mambo yatarajiwayo’. Basi, jiometria ya YANTRA DHAMMA ni ufunguo wa ‘Imani’ na ‘Matendo’ ya ‘Mitume’ wa ‘Mambo ya Nyakati’--Kitovu cha 13 hukadirisha ‘Uhaisho na Uisho’ wa yote katika MAGEUZI na MUINGILIANO wa NIA, UFAHAMU na UZIMA—Fanusi ya ‘UFAHAMU KRISTU’.

Udhamirifu, jitihada na Matendo ndiyo misukumo ya kimifumo ambavyo nguzo kumi na mbili za ‘imani’ na ‘matendo kwa ‘mambo yatarajiwayo’ hukadirika kwa ncha za (1) Pendo ‘AGAPE’ Litumikialo (D), (2) Moyo wa Uelewa (J), na (3) Uhakika (T); halafu (4) Moyo furaha (D), (5) Moyo wa Kutoa (J), na (6) Subira (T);

halafu (7) Moyo wa Kina (D), (8) Huruma (J), na (9) Ujasiri (T); kisha (10) Uono (D), (11) Hekima (J), na (12) Ujazi (T).

Nguzo kumi na mbili (12) za ‘Imani’ na ‘Matendo’ kwa ‘Mambo yatarajiwayo’ ni zenye ‘kusitirika’ katika MRABA ALMASI na MRABA DHAMMA. Kwa mintarafu ya hivi, vekta dhamirifu zilizo wazi upeoni mwa macho ya ya mchunguaji katika Yantra Dhamma ni zenye kuwakilisha ‘MATANUZI’ ya ‘KIMIONGOZO’; asili ya (1) **Msalaba wa Ukadinali**, usiyo na mwisho, katika yote, (2) **Mwezi na Nyota yake** vifanyanvyo ‘Nuru Halisi’ ama/na ‘Mwangaza Muakisiko’ kwa ajili ya fahari, hadhi, na daraja la Usentienti wa UTU/MALAIKA (3) **Mboni AJNA** ya uweza wa kuona kote na mote penye miili ya uweza, nguvu na Utukufu, na (4) **Swastika** ya ukadirisho wa yote kuwa ni chembe duara katika mapana na marefu yenye kutanuka na hapo hapo kujizungurusha.

Katika Yatra Dhamma, Msalaba na Swastika ndiyo khasa siri ya ‘Nyakati’ na ‘Vikomo’ vya Miili ya Uzima—Matriksi. Kiuono na Ufikirifu mifumo, dhahiri yote ni ‘Kumbukumbu’; Kila wazo, dhamira na tendo huhuluku, kuunda ama kuumba ‘jambo’ pahala fulani katika usupasha-wakati. Kwa mintarafu ya haya, duara na mstari katika ualama wote mzima ya Yantra Dhamma ni fumbo la imani kwa ‘Mapenzi Mema’ na ‘Unyoofu’ katika ‘kusudi’ la UTU na MATENDO. Kiufundi, duara mbili zenye kugusana, ikiwa zitashiriki kitovu kimoja cha mapana ya duara la ‘Mapenzi’ na tena seti ingine duara mbili, basi kutafanyika sura na utukufu wa ‘chotara nne’ zifanyazo cha za mraba wa miongozo...

kufanyika sura na utukufu wa ‘chotara nne’ zifanyazo cha za mraba wa miongozo ndiyo khasa asili ya ‘mraba’ na ‘Msalaba Ngazi’ ukadirishao ‘Swastika’. Kwa mintarafu ya hili, Trizaniumu ni

ufunguo wa kuyabaini yote katika ulimwengu wa sura na nishati. Basi ndiyo yawa, jicho mashoto la Horasi huhusisha fahamu zote 'sita' za UTU, kuonja-kunusu-kugusa-kusikia-kuona-kufikiria, ilivyo ni muktadha wa 'milango ya fahamu' katika Ufahamu; mambo yajayo ya 'mwangaza muakisiko' kwa ajili ya fahari, hadhi, na daraja la Usentienti wa UTU/MALAIKA. Tena ndiyo basi, Trizaniumu ni fumbo la imani lenye kukamilishana na 'Mboni AJNA' katika 'Duara na Nukta' za Ufahamu.

Kukamilishana kwa 'Mboni AJNA' katika 'Duara na Nukta' za Ufahamu ndiyo hasa asili ya 'Nyota ya Daudi' na 'SASA-NIA' ya UTU kwa mujibu wa muktadha akilifu wa Ontolojia ya Taasisi-Uono-Jitihada/Matendo/Matendeko. Kiufundi, 'Duara na Nukta' ndiyo kile Buddha alifundisha kuhusiana na 'Samma Samadhi'-- umbonishaji wa fahamu; ndivyo basi hili ndiyo khasa asili ya 'Duara ndani ya duara kwa uhamonifu wa skeli dayatonishi' vyenye kushiriki kitovu kimoja. Kiuno na ufikirifu mifumo, duara ndani ya duara ni ukadirisho wa 'utonali wa fahamu' ambavyo 'zabibu 13 za usentienti/kujisikia', panapo fanusi ya 'nyota ya Daudi', hukadirisha 'kujisikia kana kuishi katika wakati wa sasa' na tena 'wakati kusonga mbele'...

Kujisikia kana kuishi katika wakati wa sasa, kiuono na ufikirifu mifumo, ni athari ya Kisamsara na Maya; kwa kuwa SASA-NIA ni jiometria KUBU ya ufahamu ambavyo 'Dhahiri' ni 'Kumbukumbu' ya fizikia na metafizikia ya UTU na KUJICHAGULIA katika miili ya uweza, nguvu na utukufu. Kwa mintarafu ya hili, kujitambua ni kujiwazia UTU katika fizikia na metafizikia ya UZIMA WOTE/UZIMA WA MILELE. Basi ndiyo yawa, mambo ya ufahamu na kujitambua yana muktadha wake uliositirika, ELIMU 3.0: ILIMU ILIVYO NI METAFIZIKIA YA ELIMU.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=6f-DAVQ-Rmw>

=====

## **SEHEMU YA PILI: FUNGUO ZA ‘MAARIFA YA KAZI’**

### **Metafizikia ya Mifumo: SASA-NIA ilivyo ni kitovu cha Ufahamu Mkuu na Uweza**

SASA-NIA ilivyo ni ‘jiometria KUBU ya ufahamu’ ambavyo ‘Dhahiri’ ni ‘Kumbukumbu’ ya fizikia na metafizikia ya UTU na [KUJICHAGULIA katika miili ya uweza, nguvu na utukufu](#); kheri ya Elimu 3.0, ndiyo ufunguo wa ‘mawezekano yenye kupitiliza kawaida’.

Kwa mfano, kwa kadiri dhahiri yote ni ‘kumbukumbu’ katika SASA-NIA upo uwezekano wa kuona mambo katika ‘mapana mengine zaidi ya wakati na uwepo’. Kwa mintarafu ya hili, kuona mambo ya jana, pembeni ya leo, kesho kiwakati ni uwezekano kwa kuwa inategemea na ‘[MUONA anajiwekaje](#)’ ili kuyaona yaliyo kwenye ‘Samsara’ na ‘Maya’.

Kiufundi, samsara na Maya ni NIA na MATOKEO ya mikondo ya KUJICHAGULIA JUMUISHI na MATENDO/MATENDEKO. Basi ndivyo yawa, kwa rizayati ya [MKIA KUBU-MAGEUZI](#), ushuhudiaji wa kupitiliza ‘mbingu na Nchi’ ni uwezekano.

[Ushuhudiaji wa kupitiliza ‘mbingu na Nchi’](#) ndiyo khasa asili ya nyoka wawili wanaojisokotea katika mhimili, [Gongo kwa Msafiri](#), na

vile vile ‘Mbawa za Kupaa Mbinguni’ katika topografu-picha ya Kusini ya Yantra Dhamma; ambayo ni topografu ualama wa KUJICHAGULIA.

Kwa mintarafu ya hivi, Nyoka wanaojisokotea ndiyo hukadirisha ‘Umbonishaji wa fahamu’ katika ulimwengu wa dhahiri; mapana ya ‘ualogarithimu/eksiponesha’ ndiyo hasa asili ya ‘utonali wa fahamu’ na vile vile kadiri moja hata ingine ya ‘Duara ndani ya Duara’ kwa UONO KUTOKEA JUU YENYE MBAWA—fahamu ya hisia za mwangaza kwa rangi Saba (7) za Upinde.

Kuyafahamu haya kwa kina ndiyo ufunguo kwa ajili ya UELEWA juu ya ujuzi na ujenzi wa Jamii/Taifa/Dola/Himaya n.k.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=a29vuAxfox4>

=====

### **Shika Neno, Tenda Neno: Ualama na Matendo kwa Wanajamii**

Shauku ya jamii/jumuiya yoyote inawezakufungamanishwa na Ualama na Matendo kwa ajili ya ‘Kudra na Kheri zake’ ili kakadirisha mapana ya mbegu za Wakati-Jamii-Machaguo ya Kitaasisi-Matukio.

Ualama na Matendo ni asili ya ‘mafikara’ na ‘dhahiri’ kuhusiana na mtu/jamii/taifa/mataifa/dola katika ‘kusudi’ la UTU na Kujichagulia.

Kiuono na Ufikirifu mifumo, muktadha akilifu wa ‘[Matendo ya Mitume](#)’ ni fizikia na metafizikia ya KUBU ilivyo ni Metakubu. Umetakubu ni ‘unje ndani’ wa kubu-fizikia ambavyo ni ‘Msalaba’ wa ‘mapana na marefu ya wakati’ kuelekea kitovuni pa ‘[Usiwakati](#)’; Umetakubu hukadirisha ‘kweli na fahari’ ya ‘Kujiwazia Utu’--Udhamirifu, Jitihada na Matendo/Matendeko. Basi ndiyo yawa, ‘mambo ya ufunuo ni mambo ya pahala pasipo na wakati tena’--‘kawaida’ ipitilizayo ‘kawaida tuliyoizoea’...

Kwa mintarafu ya haya, kiuono na ufikirifu mifumo, Taifa lolote ni ‘Taasisi’ kadiri vile vile, kwa mfano, ‘[Kanisa ni taasisi](#)’. Tofauti ya ‘Taifa’ na ‘Kanisa’ ni utowepo ama/na uwepo wa ‘umetakubu’ wa miili ya uweza, nguvu na utukufu katika muktadha akilifu wa ufungamano wa ‘kusudi’ la ‘matendo/matendeko’. Basi ndiyo yawa umetakubu ndiyo asili khasa ya ‘Metafanusi’--udhamirifu, jitihada na Matendo wenye kheri katika mapana yenye kupitiliza wakati. Tena basi ndiyo yawa, udhamirifu, jitihada na matendo katika [metafanusi ya ‘kujiwazia UTU’](#) huleta hata uwezekano wa ‘[kuukomboa wakati](#)’.

Yantra Dhamma ni ufunguo wa unje-ndani wa pendo lenye kuyashikilia yote—mapana-marefu-kimo-kina ilivyo ni ‘[Ufahamu Kristu](#)’. Kiufundi, kanisa ni kheri, baraka na fanaka ya udhamirifu, jitihada na matendo wa UTU kupitia [metafanusi ya ‘UFAHAMU KRISTU’](#). Kwa mintarafu ya haya ushiriki wa ‘kusudi’ katika miili ya uzima ndiyo hukadirisha utukufu wa dhahiri kwa kadiri ya ‘unyoofu’ na ‘mapenzi mema’ ikiwa jamii na wanajamii wanatafuta ‘mwangaza’ kwa ajili ya hatma ya nia na matendo yao.

Ujenzi wa nchi-taifa, una kheri ikiwa miongozo yake ya UTU na Kujichagulia ina (1) Udhamirifu, (2) Jitihada, na (3) Matendo kwa

ajili ya ‘UTU Bora’. Sasa, Je, UTU Bora huja vipi katika ususi na ufumaji wa jamii na taasisi zake?

Duniani leo hii, Agosti 2024, hakuna hata taifa moja lenye ‘ukweli’ na ‘fasaha’ ya Nia na Matendo ya kuyakinisha ‘UTU Bora’ khasa; Kwa mintarafu ya hili, muktadha wa ‘Shika Neno, Tenda Neno’ una ‘mapengo ya kiufahamu’ na kujua isivyobora.

Nchi ya Merekani, kule Amerika ya Kaskazini, pamoja na yote yanayokadirisha kujipambanua Uweza, Nguvu na Tawala; kiuono na ufikirifu mifumo, hali halisi ya utamaduni na maendeleo yake una mema kwa mabovu mengi.

Nchi ya Merekani, kutajwa ni ya demokrasia maridhawa; kiuono na ufikirifu mifumo, bado haina ‘roho’ ya kheri bali kimvuli mwangaza kisichotimilifu kwa ukweli halisi mambo. Kwa mintarafu ya hili, muktadha akilifu wa utamaduni wa nchi-taifa ndiyo hujinasibu na demokrasia kama (1) ‘uhuru wa kujidhirisha mapenzi ya utu’ na (2) ‘kujichagulia’—japo uhuru, kwa nyookeo wa kweli yote ya miili na uzima, ni ‘kazi’. Basi ndiyo yawa, kazi ni shughuli ya pumzi, jitihada na matendo—ikiwa haya yana umetakubu sahihi wa kujiwazia UTU bora, jamii huwa na chachu ya kweli ya maisha yenye kheri ya utangamano.

Nchi ya Merekani, kutajwa ni nchi ya waliohuru—nchi ambayo yoyote anaweza kukaribia ndani na kuja kuwa vile apendavyo na kutaka ilivyo ni udemokrasia. Kiufundi, kujichagulia ni zao la udhamirifu, jitihada na matendo—kule Merekani, hili lilitengenezewa shauri la muongozo kwa ajili mwanajamii na nchi-dola kama utamko wa mastahiko haki kumbaizi kwa ajili ya (1) Udhamirifu wa Furaha, (2) Uzima, na (3) Liberti... Basi ndiyo yawa,

utonali wa fahamu ni mambo ya ushiriki wa hisia na kujisikia kijamii kama ‘mwili mmoja’.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=xUF8ULpxN8Q>

## **Ualama Taasisi: Ufunguo kwa Maagano ilivyo ni ‘Upepo’ na ‘Maji’ wa UTU**

Ushiriki wa hisia na kujisikia kijamii kama ‘mwili mmoja’, kiuono na ufikirifu mifumo, ndiyo ufunguo wa taifa moja kama taasisi; Kutokea ‘usikitu’ hadi kuja kuwa ‘kadiri ya kitu’ ni muktadha akilifu wa ‘Ontolojia ya Taasisi’. Kwa mintarafu ya haya, uimajinishi jamii hugemwa ukunjufu wa kheri na kudra kupitia ‘alama za ujamii’ na ‘Matamaniao’; Merekani kwa mfano, Matamaniao ndiyo khasa ule muktadha wa kuitaja ‘Ndoto Amerika’--fursa kwa wote katika nchi ili kupata uweza wa kukua na kustawi kiuchumi; [nchi ambayo mtoto yeyote aweza kukua na kuja kuwa ‘Rais wa Nchi’](#)-- ‘anga si kikomo’...

Nchi ya Merekani, kutajwa ni nchi ya wanabidii kwa ajili ya kuyatafuta mafanikio, kwa mujibu wa yale yote yaliyotengenezewa utaratibu wa kinchi-taifa, ni mambo ya mkono wa kushoto na kulia kwa Yantra Dhamma. Kwa mintarafu ya hili, muktadha akilifu wa ‘udemokrasi’ na ‘ujamhuri’, kiufundi, ni mambo ya ‘mapana ya utamaduni’ na ‘mapana ya mipaka ya nguvu za ushawishi kidola’. Basi yawa, harakati zote za kisiasa juu ya hisia na kujisikia kiutaifa, Merekani, hizo hujipambanua kwa ‘sauti ya umoja’, tuseme kichama, juu ya mustakabli wa nchi-taifa kwa spektramu ya ‘mlengo wa kushoto ama/na kulia’ wa kujiwazia ‘Uzalendo’. Kinachoshiriki nafasi kwa maduara yote mawili ya mlengo wa (1) kushoto/uradikali, na (2) mlengo wa kulia/Uhifadhina, ni

muktadha akilifu wa mapana ya jamii (1) kimaslahi na (2) ustawi katika/kupitia utaasisi wa demokrasi ya kiliberali.

Bidii kwa ajili ya kuyatafuta mafanikio, kwa Merekani, ndiyo huja na ualama wa 'Nyota' na 'Makundi ya Nyota'. Kiuono na ufikirifu mifumo, na basi muktadha akilifu, nyota ya pembe tano ni ushahibiano na 'Mtu/UTU'; na hali, nyota ya pembe sita (Nyota ya Daudi) ni alama 'UTU katika MFUMO'. Basi yawa ndivyo Amerika, Merekani, Bendera yake ni ualama wa 'Nyota Nyingi'(50 : 6-5-6-5-6-5-6-5-6) na Mistari ulali ipatayo 13 (Nyekundu/Miupe); ambavyo kiuono na ufikirifu mifumo, kuna muktadha akilifu wa watu, majimbo kuoana na udhamirifu, jitihada na matendo.

Kiuono na ufikirifu mifumo, Kujisikia ni 'mambo ya upepo' na hali matukio ni 'mambo ya maji'--maji jinesesia; Kwa mintarafu ya hivi, Usemi wa kwamba 'Bendera hufuata Upepo' una muktadha akilifu na yote yenye asili ya tuseme 'Siasa na Maoni' kwa kuwa maoni ya wananchi/wanajamii huwakilisha hisia ama/kujisikia kwao kwa wakati. Basi ndivyo yawa, siasa na maoni huakisi UTU ama/uzalendo wa mwanajamii/mwananchi kwa kadiri ya 'chachu ya utaifa' na pia miongozo yake.

Kiuono na ufikirifu mifumo, Kujisikia ni 'mambo ya upepo' na hali matukio ni 'mambo ya maji'; Kwa mintarafu ya hivi, Bendera hupepea ikiwa imesimama barabara juu ya sura ya nchi ilivyo, kimuktadha akilifu, ni jambo pacha na 'msimamo wa kijamii'. Mambo ya miegamio/misimamo ya kijamii ndiyo huja na 'Nembo za jamii/taifa/dola/himaya n.k kwa ajili ya kusadifu udhamirifu, jitihada na matendo.

Merekani kwa mfano, nembo yake ya kitaifa ni yenye ualama wa Ndege Tai aeleaye kuruka juu angani huku akiwa ameshikilia kwa miguu yake—mishale 13 (kulia) na jani la Mzeituni(Kushoto). Kwa uono na ufikirifu mifumo, ndege tai ni ndege wa mawindo kwa hivyo utaifa, kwa alama ya ndege huyu, hujinasibu na hulka ama silika ya ‘mawindo na uviziaji’ kwa ajili ya kujichagulia na ustawi wake—mawindo na uviziaji kuwa muktadha akilifu wa ‘Udhamirifu’.

Merekani kwa mfano, nembo yake ya kitaifa ni yenye ualama wa Ndege Tai aeleaye kuruka juu angani huku akiwa ameshikilia kwa miguu yake—mishale 13 (Kulia) na jani la Mzeituni (Kushoto). Kwa uono na ufikirifu mifumo, mishale 13 na jani la mzeituni ni ualama kwa ajili ya mataraji ya ‘Vita/Kujihami’ na ‘Amani/Fanaka’. Kwa mintarafu ya haya, namba 13 huchukua nafasi ya kipekee katika ualama wa Taifa la Merekani ambavyo ile ‘mistari la ulali’, ipatayo 13, kwenye bendera huja kuwa ‘mistari wima’, ipatayo 13, ya dhamira, misimamo na kujichagulia. Basi yawa tena, Nyota 13 juu ya Ndege Tai ni muktadha akilifu wa ‘UTU/TAIFA katika MFUMO’--mfumo wenye kujinasibu ‘utukufu’ wa mageuzi ya kimbingu na nchi.

Merekani kwa mfano, nembo yake ya kitaifa ni yenye ualama wa Ndege Tai aeleaye kuruka juu angani huku akiwa ameshikilia kwa miguu yake—mishale 13(Kulia) na jani la Mzeituni(Kushoto). Kwa uono na ufikirifu mifumo, muktadha wa akilifu kwa ajili ‘kujichagulia’ na ‘ustawi’ husukumwa na dhamiri ya kujipambanua ‘Kijeshi’ na ‘Kazi’ katika mapana ya nchi ambavyo kitendo cha Ndege Tai kutokuwa amejishikilia popote kinaakisi kutotegemea nguvu ya kingine chochote cha asili ya nchini bali ‘jitihada za mbawa katika wepesi wa hewa’ -- katika muktadha akilifu wa ‘uwepo na kusonga’.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=1kxXgGtFvAk>

=====

## **Amerika hata Tanzania: Marejeo ya Nia na Misingi ya Nchi na Tawala**

Kiuono na ufikirifu mfumo, muktadha wa Ndege Tai unajitokeza kama ‘Ngao ya Ustawi’ yenye Pembe za Ndovu zipatazo mbili (2), upande wa kuume na kushoto, na tena juu ya Kilele cha Mlima Kilimanjaro. Kwa mintarafu ya haya, Tanzania kama taifa la watu muktadha wake wa kitaasisi katika kujichagulia matunda yake ya udhamirifu, jitihada na Matendo unasadifiwa na ‘Uthabiti wa Uzito’ wa maliasili/mali-akili kwa ajili ya (1) Kulijenga taifa, na (2) Kulilinda Taifa.

Kiuono na ufikirifu mfumo, muktadha wa ‘Bibi na Bwana’ ni uakilifu wa (1) Jitihada, na (2) Ukesha Macho kwa ajili ya Dhamiri, Nadhiri na Uzingatiaji wa Miiko ya Mila, Desturi na Jadi ya wananchi walio ni wenyenchi. Kwa mintarafu ya haya yawa basi: (1) mila ni mwenendo wa sura za kimatendo--matendo ya kimazoea katika taratibu zinazokubalika/kuridhiwa na jamii yote; (2) Desturi ni namna ya kuyaendea/kuyatekeleza matendo kwa kadiri ya nyakati na mpangilio wa mambo, na (3) Jadi ni muingiliano wa alama oanifu zinazoshikilia funguo za ‘Shika Neno, Tenda Neno’-- nia na msimamo wa jamii katika masuala ya msingi kwa ustawi wa pamoja.

Kiuono na ufikirifu mifumo, muktadha wa shoka-mkuki-nyengo ni uakilifu wa ‘Jadi’ ambavyo jitihada kwa sura ya kujituma, kazi na uwajibikaji vinapelekea kadiri ya ‘Ustawi’ wenyekheri wa Wananchi wenye nchi. Kwa mintarafu wa haya, jadi ni jambo lenye asili ya fizikia na metafizikia ya jamii yoyote. Basi ndiyo yawa, alama za shoka, mkuki na nyengo, kiuono na ufikirifu mifumo, zina mapelekeo ya wazi na tena mengine ‘yaliyositirika’.

Mapelekeo ya wazi na tena mengine ‘yaliyositirika’, kiuono na ufikirifu mifumo, ndiyo mambo yaliyo ni ufunguo wa ‘[Gongo kwa Msafiri](#)’; Taifa changa katika kuiishi na kuidumisha na mifumo yake hukadirisha muktadha wa ‘Kujichagulia’ ilivyo ni mustakali wa ‘Uzima wake’ na hatma ‘Kujiongoza’ kwake ili kuendana na ‘mambo ya nyakati’. Basi ndiyo yawa, tunu za taifa huleta chachu ya ‘mila-desturi-jadi’ kwa taifa kwa ajili ya ‘machaguo ya kitaasisi’. Na tena basi, uono na uhakika wa kiutamaduni ni fanusi ya Utaasisi wa nchi-taifa kulingana na hisia na kujisikia—UTU na UZALENDO.

Mapelekeo ya wazi na tena mengine ‘yaliyositirika’, kiuono na ufikirifu mifumo, ndiyo mambo yaliyo ni ufunguo wa ‘[Gongo kwa Msafiri](#)’; Taifa changa lina maadui watatu wa fanusi ya umoja wake na kujichagulia—umaskini, maradhi na ujinga. Kwa mitarafu ya haya, ‘[Gongo kwa Msafiri](#)’ ni mhili wa imani na matendo kupitia ‘Nuru ya Ufahamu’. Basi ndiyo yawa, maadui hawa wawili wanaweza kukabiliwa kwa (1) ELIMU, na (2) ILIMU; Elimu ya Maisha kwa Jitihada za Masomo na Visomo ni mambo ya ‘Elimu’ na hali jitihada za kujielimisha kwa ajili ya nia na mapenzi bora na Utu ni shughuli ya ‘Ilimu’.

Mapelekeo ya wazi na tena mengine ‘yaliyositirika’, kiuono na ufikirifu mifumo, ndiyo mambo yaliyo ni ufunguo ilivyo ni ‘[Gongo](#)

[kwa Msafiri](#)’; Taifa changa lina changamoto za kimsingi katika shughuli ya kuwaunganisha watu/wanajamii katika ‘udugu’ na ‘umoja’ wa kweli kwa kuwa mapishano ya upeo, uelewa na utayari wa kudumisha ‘Uhuru na Umoja’ na basi ‘misingi ya imani’ kwa wanajamii haina budi kutaasisiwa ili kujenga kusudi la jamii/taifa/Dola. Kwa mintarafu ya haya, Mwenge wa Uhuru ndiyo hasa alama ya taifa inayohuisha na kuhaisha zana za jadi za taifa: Shoka-Mkuki-Nyengo. Basi ndiyo yawa, katika nembo ya taifa ya Tanzania, Shoka-Mkuki-Nyengo huja kwa ‘rangi ya dhahabu’... ‘Rangi ya njano ya dhahabu’ ni ualama wa ‘UTU bora’/Utu wa thamani.

‘Rangi ya njano ya dhahabu’ ni ualama wa ‘UTU bora’/Utu wa thamani ambavyo ndiyo hasa hutawala robo ya juu ya ‘Ngao ya Ustawi’. Kwa mintarafu ya hili, Taifa la Tanzania limeasisiwa, kutaasishwa na kusimikwa kuwa ‘Taifa la Wateule’. Kiuono na ufikirifu mifumo, kuwa ‘Taifa Teule’ ni zao la zindiko sahihi la utu na kujichagulia ambavyo ‘Imani’ na ‘Kusudi’ la wananchi wenye nchi linajengewa uwezekano wa kiustawi na kheri ili kufaa ‘Jaala’ ya ‘Utukufu na Nguvu’ wa kile KILICHO NI KHASA asili ya uweza na uzima wote wa kimiili. Basi ndivyo yawa, kiuono na ufikirifu mifumo, ‘Mungu’ ni muktadha akilifu kwa kile KILICHO NI KHASA asili ya uweza na uzima wote wa kimiili—miili ya uzima yenye kuonekana na ile isiyoonekana.

Zindiko sahihi la utu na kujichagulia ambavyo ‘Imani’ na ‘Kusudi’ la wananchi wenye nchi huweza kutaasishwa, kiuono na ufikirifu mifumo, ndilo utundu na ufundi wa kubuni alama za utaifa na kuzifungamanisha na miongozo ya kimifumo, sanaa na utendaji. Kwa mintarafu ya hili, Udhampirifu wa ‘Kheri’ na ‘Fanaka’ ya nchi ndiyo huifanyizia sura ile sanaa za bendera na nembo kwa ajili ya wale wote wenye nasibu ya ‘hekima’ na tena nasibu ya ‘Haki’

wabahatike kuotea msingi ya nchi na tawala ‘pasipo kulazimishwa’—ila subira na saburi na kulitambua kusudi la utaifa/mataifa na tena kadiri ya upevu wa akili na hisia.

‘Imani’ na ‘Kusudi’ la wananchi wenye nchi huweza kutaasishwa kisanaa, ambavyo kiuono na ufikirifu mifumo na tena kwa mfano, ndilo utundu na ufundi wa kubuni bendera ya Merekani kuwa na mistari 13—mistari hiyo hiyo ipatayo kumi na mitatu (13) inajitokeza katika [nembo ya taifa na kukaziwa na mishale 13 na Nyota 13 juu ya Ndege Tai](#). Kwa mintarafu ya hili, la hadharani laweza kuwa rejeo la majimbo 13 ya awali katika ushirikisho wa mataifa; japo kwa muktadha akilifu uliositirika ni ‘Sala ya Mageuzi’ ya kiutu, ustawi na utamaduni. Basi ndivyo kuwa, (1) Ngao (Vesika Paisisi) ya ustawi, na (2) Nyota ya Daudi, na (3) Mwezi na Nyota, na (4) Msalaba, ni alama jadi zenye asili moja – baraka/vishikizo imani ama/na ‘hifadhi takatifu ya tunu za udhamirifu wa utu bora’ kwa ajili ya kuwazia mema ya nchi.

Bendera huwa na mistari, rangi na sanaa kwa ajili ya ‘hisia na kujisikia’ -- kwa muamko wa wanajamii wanaowakilishwa na hiyo yenyewe. Kwa mintarafu ya hili, ufundi wa ubunifu wa sanaa za bendera na nembo huhusisha hata maarifa na maarifu ya Elimu 3.0: Ilimu ilivyo ni metafizikia ya Elimu. Basi ndiyo yawa, usanifu unaotawala bendera nyingi ni sehemu ya kadiri ya ‘Yantra Dhamma’--[visahani, mistari chali, mistari wima, vipande vya almasi, Nyota ya Daudi, misalaba, Mwezi na Nyota, Chanja Mkasi, Mikatizo/ukashata, Vesika Paisisi, Jua, Ndege](#), na vile vile viumbe vya ngano—[joka/tai-vichwa viwili/farasi Upembe](#) n.k.

Bendera huwa na mistari, rangi na sanaa kwa ajili ya ‘hisia na kujisikia’ -- kwa muamko wa wanajamii wanaowakilishwa na hiyo

yenye. Kwa mintarafu ya hili, kutamalaki kwa rangi (1) Kijani, (2) Njano, na (3) Nyekundu katika nyingi ya Bendera za mataifa ya Kiafrika ni ‘ishara ya jambo’; kadri vile vile rangi (1) Nyekundu, (2) Nyeupe, na (3) Bluu [kujirudia rudia kwenye nchi za Ulaya na hata Amerika.](#)

Bendera huwa na mistari, rangi na sanaa kwa ajili ya ‘hisia na kujisikia’ -- kwa muamko wa wanajamii wanaowakilishwa na hiyo yenye. Kwa mintarafu ya hili, kiuono na ufikirifu mifumo, [bendera kama ya taifa la Israeli kuwa na ‘Nyota ya Daudi’ na halafu mistari yenye kuisindikiza alama hiyo ya kati kati, iliyo juu na chini, ni ‘fumbo la imani’ la baraka la ‘kheri ya mbingu na nchi’--kwenye Yantra Dhamma, mistari hiyo ndiyo ile hasa inayojitokeza kwenye alama ‘hashi/reli’: Wa juu huleta ‘Ushindi’ na wa chini ‘Huzindika nchi katika uthabiti wa Imani, Jitihada na Kujichagulia’.](#) Basi ndiyo kwa Afrika, [nchi inayotumia ualama wa ‘Nyota ya Daudi’ ni Burundi ambavyo kisahani cha utatu wa Nyota za Daudi hukaziwa na chanjamkasi](#) ya rangi nyeupe.

Kutamalaki kwa rangi (1) Kijani, (2) Njano, na (3) Nyekundu katika nyingi ya Bendera za mataifa ya Kiafrika, kiuono na ufikirifu mifumo, ni ‘ishara ya jambo’ la ‘uchanga’ na matayarisho ya kiutu yajayo na ‘Udugu’ na ‘Uhuru’. Kwa mintarafu ya hili, ndiyo hata kwa hapa Tanzania, Kwenye Ususi wa Dola/Utaifa kwa sanaa na michezo, timu ya Yanga huwa na rangi hizi (1) Kijani, na (2) Njano ambavyo ‘watani wake wa jadi’, klabu ya Simba, huwa na rangi, (1) Nyekundu, na (2) Nyeupe. Basi ndiyo yawa, Yanga ni Klabu yenye kusadifu ‘Waafrika Wachanga—Young Africans’--wachanga kiutaifa; Simba ni muakisiko wa Waafrika waliokomaa, kujitawala na kujenga mapana ya fahari ya Uisho kwa ajili ya Utu wao bora.

Rangi (1) Nyekundu, na (2) Nyeupe. Kiuono na ufirifu mifumo, ni rangi za kuchochezi wa dhamiri na jitihada. Kwa mintarafu ya hili, [‘Jogoo wa Kazi’ ndiyo huja na usemi: ‘Daima Mbele, Nyuma Mwiko’](#). Kule nchi kaka ya Tanzania, Kenya, Jogoo huyu huonekana kashika shoka kwa mguu moja—alama ya wito na ukumbusho kana : ‘Sasa Kumekucha’, tuinuke kufanya kazi ya kulijenga taifa. Basi ndiyo yawa, Kenya ni nchi yenye ‘ncha ya pili’ ya chachu ya utu bora, ncha ya kwanza iko Tanzania: Uhuru ni Kazi kwa mchakato wa shughuli za ‘Jembe na Nyundo’ na wakati mmoja wa ukomavu—iwe kwa ‘Shoka na Nyengo’. Basi ndiyo, kwa Tanzania kipindi cha ‘Tumaini’ ni kwa ajili ya ‘Matayarisho na Kujijenga’ ili itangamanishe mataifa yote ya Afrika kwa ‘kulishiriki kusudi fulani’ na nchi ya Kenya.

Alama za mkuki, kwenye nembo za taifa/mataifa, kiuono na ufikirifu mifumo, ni muktadha akilifu wa [‘Ulinzi’](#) wa ‘Ustawi wa Jamii’--Kwa nchi ya Kenya, [Simba Wawili wenye kujishikiza na ‘Ngao ya Msimamo’ na ‘Mikuki’ – kikuki iliyokatika mtingo wa ‘Shika Neno, Tenda Neno\(X\)’](#) ipo kuwakumbusha wale wote wenye hekima na busara juu ya ulazimu wa kuilinda mifumo yote maisha kwa ujasiri na fahari kuu. Uhuru/Usovereini bila Ulinzi ni Kazi-Bure, basi ndiyo yawa, kuna yale ambayo kule Kenya ‘hawajaanza nayo’ na ni ‘deni’ kwao kiustawi: Umuhimu wa chachu ya ‘Udugu na Uhuru’ wa kweli kwenye nasibu ya taifa lolote changa... Tena ndiyo basi, Chama cha Makutaniko ya ‘Wananchi wenye Nchi’ – wa kutokea kule Africa ya Kusini, [chama cha ANC](#), wana ‘ushahidi wa alama za ufunguo wa hatma’ za ‘Simba na Yanga’...

Chama cha ANC, hutumia [nembo iliyo ni](#) (1) Ngao, (2) Mkuki wa Taifa, (3) Bendera yenye Rangi ya Njano ya dhahabu, Kijani na Nyeusi, na (4) Gurudumu la kusongambele katika utu bora na jumuishi—[Gurudumu la Dhamma!](#)

Mambo ya ‘Upepo’ na ‘Matukio’, kiuono na ufikirifu mifumo, ndiyo asili khasa ya ule ufundi/utundu wa utayarishaji wa habari wenye kuanza na ‘habari za siasa’, tuseme kwa mfano katika gazeti--kwenye ukurasa wa kwanza, na kumalizia na habari za ‘michezo’. Kwa mintarafu ya hili ‘mambo ya siasa za ncha na tawala’ huja na ‘MRABA wa MAISHA’--Meza ya ‘Wakati-Jamii-Machaguo ya Kitaasisi-Matukio’ ambavyo [Siasa na figisu](#) ‘husukumia mapana na marefu ya akili kwenye kitovu’ vya wigo ama/na vina vya mafikara na upeo. Basi ndiyo yawa kinyume na kufuma na kuyafumua mawazo ni hisia za furaha zijazo na ‘habari za michezo na burudani’--’kuondoa stresu ya kiakili’. Habari za duru za michezo na burudani zinaweza kutumika kufunika ‘Upepo Mbaya/Mzuri’ wa kimatukio ya kisiasa na utawala kwa jamii inayosombwa kirahisi na ‘misokotoleo ya nje kihabari za mchongo ama/na kutumbuiwa’...

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=5YMUlEsH2iI>

=====

### **Uzao wa Mzabibu na ‘Ndoto ya Ujamaa’ wa kweli**

Upepo na Matukio, kiuono na ufikirifu mifumo, ni muktadha akilifu wa ‘Sura na Mienendo ya Jamii’. Kwa mintarafu ya hili, kuna namna mbili za kukadirisha muktadha akilifu wa kheri ya ‘mapana ya jamii’ kwa uono na ufikirifu mifumo, (1) Sura na Mienendo ya Jamii, na (2) Sovereini Jumuifu. Basi ndiyo kwamba Nchi ya Tanzania, kiuono na ufikirifu mifumo, ili taasishwa kwa kusudi la kheri ya ‘Sovereini Jumuifu’ ambayo [Mwalimu Kambarage Nyerere alikuwa ‘Mtume’ na ‘Kuyatekeleza Matendo ya Mitume’ kwa kuazimia, na tena kupitia udhamirifu jitihada na matendo, taifa la watu wanaoishi kuitafuta ‘Haki’ na ‘Amani’ katika ulimwengu usiyo na ukamilifu –bado kuwepo](#) .

Ujamaa wa kweli, kiuono na ufikirifu mifumo, ni [safari ya imani ili kuiishi hakika ya mambo yenye kheri na fanaka ya jamii](#). Kwa mintarafu ya hili, taifa changa ni kisawe cha ‘Merikebu ya Wasafiri’ katika bahari yenye mawimbi na nasibu ya dhoruba. Safari salama ni fanusi ya (1) Utulivu wa wasafiri, (2) Unahodha na (3) Shughuli ya Mabaharia; na basi pia kule kujizatiti na safari yenyewe. Aidha mambo ya hao wote watatu, watatu katika moja, hutegemea sana imani na uhakika wa umahiri wa ‘mabaharia’ katika kukisafirisha chombo pasipo kupoteza uelekeo ama kuyumbishwa na ‘pepo’ na ‘mawimbi’ ya bahari.

Metafo ya ‘Mabaharia-chombo-wasafiri’ ni muktadha akilifu wa simile ya ‘Wasafiri-Serikali-Dola’; na basi uchanga wa safari yoyote ya utaifa hubakia ni muktadha akilifu kwa ‘Fanusi Tumaini’ kwa ajili ya Muelekeo wa Mashariki ya Pambazuko la UTU Bora.

Mabaharia; na basi pia kule kujizatiti na safari yenyewe, kiuono na ufikirifu mifumo, ni maombi/sala kwa ajili ya ‘rehema’ na ‘fadhili’ vijavyo na KILICHO NI KHASA asili ya uweza na uzima wote wa kimiili. Kwa mintarafu ya hili maisha daima ni safari ya kupitia yanayojulikana/kutarajiwa na yale yasiyojulikana/kutarajiwa.

Kiufundi, [mikakati ya uiisho ya chombo](#)-- chombo chochote cha wasafiri hutegemea [fizikia](#) na metafizikia ya jamii. Basi ndiyo yawa, ‘taasisi ya kidini’ daima huwa ni moja ya Nguzo ya Usalama na ‘Udau wa Amani’ wa nyumba yoyote inayojengwa; ama sivyo kigezo cha ‘kutotabirika kwa safari’ huongezeka sana’ katika jumuiya ama/na ujumuiya wa kimataifa. Kwa mintarafu ya haya, jamii na [wanajamii wanakheri ikiwa ‘Wanajielewa’ asili ya Utaifa/Dola wao;](#)

kubarikiwa upeo wa kumaizi Ontolojia ya Utaasisi wao kama ‘Ujamhuri’.

Kiufundi, [mikakati ya uiisho ya chombo](#)-- chombo chochote cha wasafiri hutegemea [fizikia](#) na metafizikia ya jamii. Basi ndiyo yawa, ‘Mtu mwenye kufahamika/kutajwa ni Yesu’, katika hali ya kusitirika, ni moja ya Nguzo ya Usalama na ‘Udau wa Amani’ kwa mataifa yote Duniani hata leo hii, Agosti 2024; mdau wa ‘Maarifa ya Kazi’ ili kukadirisha kheri za ‘Imani’, ‘Tumaini’ na ‘Mapendo’-- Duniani kuwe na Amani, Mapenzi Mema na Furaha. Basi ndiyo yawa, ili ukweli na fasaha ya hili idhihirike, kuna ‘maarifa’ na habari za ‘maarifu’ vyabidi kuzungumzwa taratibu na tena hatua kwa hatua ili kuifanikisha shughuli ya ‘Mavuno’.

Kiufundi, [mikakati ya uiisho ya chombo](#)-- chombo chochote cha wasafiri hutegemea [fizikia](#) na metafizikia ya jamii. Basi ndiyo yawa, Maarifa ya Karata Dume Shupaza juu ya Ujenzi wa Nyumba, ujumbe kwa Mabaharia, Dola yoyote ni Utaasisi/shughuli ya maandalizi ya kijamii – maandalizi yenye kukadirisha muktadha akilifu ulio ni [‘Fanusi Tumaini’](#). kwa ajili ya Muelekeo wa Mashariki ya Pambazuko la UTU Bora—Utu bora kwa wanajamii/mataifa yote. Kwa mintarafu ya haya, nyumba yoyote imara hujengwa kwa ushirikiano wa wajenzi na wakazi wenyewe. Basi ndiyo yawa, mambo ya ushirikiano yanahusisha ‘fizikia’ na pia ‘metafizikia ya mambo’ ili kukadirisha mawezekano ya ‘Hakika’ na ‘Kheri fulani’ katika mapana ya jamii na nyakati zake...

‘Kheri fulani’ katika mapana ya jamii na nyakati zake, kiuno na ufikirifu mifumo, ndiyo asili ya ‘MRABA wa MAISHA’ kuwa ni [‘meza ya utandu wa kitamaduni-- ya jamii moja jumuiifu’](#); yenye kuwambwa na ngozi ya ustawi wa jamii wenye mapana ya ‘Wakati-

Jamii-Machaguo ya Kitaasisi-Matukio'. Basi ndiyo yawa, kwa nchi ya Tanzania ingilio la [‘fanusi Imani na Tumaini’](#) imetaasishwa kwa [‘Ushirika wa Wananchi na Dola’](#) katika misingi ya UHURU-UDUGU-HAKI-AMANI.

Kutoka kwenye Vitabu vya Injili, tunafikiwa na shauri juu ya [‘Ujenzi wa Nyumba’](#); kiuono na ufikirifu mifumo, Nyumba ni muktadha akilifu kwa mambo ya jamii yenye kuhusiana na ‘uweza/uwezo’, ‘udhamirifu’, ‘miundo/ujenzi’, na ‘Matendo’--mfano, Taifa/Nchi-Dola. Kwa mintarafu ya haya, ndiyo mashauri ya ‘kujichagulia’ na ‘Hazina’ huyakinishia fasaha, kweli na hakika ya (1) Matayarisho, na (2) Utayari wa jambo; ili kukadirisha/kutarajia ‘matukio fulani’, kiwakati, na tena katika mapana ya ustawi wa jamii. Basi ndiyo yawa, Mipango na Utekelezaji ni mambo yenye kuhitaji upeo na vina sahihi vya uono na utambuzi; ama sivyo, ujenzi utahusika juu ya ‘mchanga’ badala ya ‘mwamba’.

Kutoka kwenye Vitabu vya Injili, tunafikiwa na shauri juu ya [‘Mpanzi aliyepanda Mbegu’](#); kiuono na ufikirifu mifumo, mbegu ni asili ya kheri na nasibu ya [‘Ontolojia ya Taasisi’](#); ambavyo UTU ni fumbo la imani kwa nasibu ya Kheri na Mema ya Nchi kupitia dhamira, mifumo na matendo. Kwa mintarafu ya hivi, mbegu ndiyo hasa ile ‘Sonafi’ yenye kuhaisha na kuhuisha ‘miili na uweza wa kibinadamu’ kwa kadiri ya (1) Hisia na Kujisikia--‘Usentienti’, (2) Akili ya Udhamirifu wa Mambo--‘Konsayansi’, na (3) Mwanga wa Nuru ya Utambuzi/Kujitambua--‘Nuru ya Ufahamu’. Basi ndiyo yawa, ‘upandaji mbegu’ ni muktadha akilifu wa nafsi ya duniani, nafsi-roho na Roho ya Uzima wote. Tena basi, sonafi ndiyo nguzo ya pumzi na uzima kwa utu—ufunguo kwa mambo ya fizikia na metafizia ya ‘kujiwazia UTU’ kupitia ‘miili ya uweza’.

Kutoka kwenye Vitabu vya Injili, tunafikiwa na shauri juu ya ‘[Uzao wa Mzabibu](#)’; kiuono na ufikirifu mifumo, Uzao wa Mzabibu ndiyo hasa asili ya ‘Vinasaba UTU’ vinavyoshikilia (1) ‘Fizikia na metafizikia’ ya ‘milli ya uweza wa kibinadamu’ na (2) Mifumo uhai ya kawaida na mifumo uhai yenye kupitiliza ‘kawaida’. Kwa mintarafu ya hivi, Metafanusi yenye kushuhudia ‘Mimi ni Mzabibu Kweli’ ni fumbo la imani lenye ufunguo wa kukadirisha ‘Kheri’ ya (1) Mifumo Uhai ya Kawaida, na (2) Mifumo Uhai yenye kupitiliza kawaida. Basi ndiyo yawa, Maisha na kuishi ni daima fumbo la imani la ‘Taasisi’ ndani ya ‘Utaasisi’ mwingine wenye ‘kuishi zaidi’. Tena basi, Uzima wote wa Miili ni Msokotano wa Dhahiri ndani ya Dhahiri nyingine hata kwenye hatma za ‘Ukitu’ na ‘Usikitu’—Mambo ya Roho wa Uzima wote.

Kwenye Yantra Dhamma, mambo ya ‘[Uzao wa Mzabibu](#)’ huja na upande wa kushoto wa ‘MRABA DHAMMA’ ambavyo Jamii ni muingiliano wa hisia tofauti tofauti na msimamo wa jamii. Kiuono na ufikirifu mifumo, hisia na kujisikia (Usentienti) ni nasibu ya watu wenye chachu tofauti tofauti ya Nuru ya Ufahamu; jambo likadirishalo /mbegu zilizoanguka kwenye mchanga, miba, miamba ama udongo mzuri. Kwa mintarafu ya hivi, UHURU-UDUGU-HAKI-AMANI ni ufunguo wa nasibu yenye kutangamanisha (1) Hisia na Kujisikia ‘usentienti’, (2) Akili ya udhamirifu wa jambo jema ama bovu ‘konsayansi’, na (3) Nishani ya Utu Bora. Kwa mintarafu ya hivi, Metafanusi yenye kushuhudia ‘Kaa ndani yangu, Nami nikae ndani yangu’ ni wito wa hiari kwa ajili ya Nishani ya Utu bora—Utu bora ujao na ‘[Vesika Paisisi](#)’ ya jamii katika chachu ya ALMASI ya UHURU-UDUGU-HAKI-AMANI. Basi ndiyo yawa, ahadi ya kuitikia wito ni: ‘Akaaye Ndani yangu, Huyo Huzaa sana.’

Kwenye Yantra Dhamma, mambo ya ‘[Uzao wa Mzabibu](#)’ huja na upande wa kushoto wa ‘MRABA DHAMMA’ ambavyo Jamii ni

muingiliano wa hisia tofauti tofauti na msimamo wa jamii. Kwa mintarafu ya hivi, Taifa na Nchi ya Tanzania, imekusudishwa Nishani ya Utu Bora ilivyo ni ALMASI ya UHURU-UDUGU-HAKI-AMANI. Basi ndiyo yawa, Maarifa ya ‘Dume la Kisu/ALMASI’ yametaasishwa katika nembo ya Taifa kama ‘[Mkuki wa Jaala](#)’; asili ya ‘akili ya udhamirifu wa mambo’--udhamirifu wenye kushiriki kitovu cha hatma ya ‘ukuwa kitu’ na ‘usikuwa kitu’ kimatakwa na mapenzi ya jamii. Matakwa na mapenzi ya jamii ni jambo/mambo yenye kuja na muktadha akilifu wa ‘Kujichagulia’-- Jadi ya Shoka na Nyengo ilivyo ni ‘Maarifa ya Kazi’. Tena basi, hatma ya nchi-taifa/dola ndiyo yawa ni ‘fumbo la imani’ linayotegemea ‘ukomvu’ na ‘Utayari’ wa Kulijenga na Kulilinda taifa kwa: (1) Kuchanja mapana ya Nchi na Mbingu, vile vile (2) Kuvuna yapandwayo katika ‘nchi’ pia jamvi la usupasha wakati—mambo ya ‘nyekundu ya udongo mzuri’ na ‘Njano ya Dhahabu ya Utu-kazi wa thamani’.

Kwenye Yantra Dhamma, mambo ya ‘[Uzao wa Mzabibu](#)’ huja na upande wa kushoto wa ‘MRABA DHAMMA’ ambavyo ‘Utu-kazi wa thamani’ ni ‘Nyota ya Utimilifu wa Miundo na Mageuzi’ kupitia ‘[Gongo kwa Msafiri](#)’. Kwa mintarafu ya hivi, Metafanusi ni asili ya miongozo yenye kheri kwa ajili ya LIBERTI-UuMOJA-UJAZI-UTANGAMANO. Basi ndiyo yawa, ‘[Gongo kwa Msafiri](#)’ ni nia ya kuondokana na ukafiri na hapo hapo kuwa faraja ya mapito katika safari; tena basi ‘Ujazi’ ni kheri ya yule mtu aliyeijenga nyumba yake juu ya ‘Mwamba wa Metafanusi ya Jamii’ ambavyo mvua na pepo vikivuma, nyumba haitetereki... [Gongo kwa Msafiri](#) ni Usanisi wa (1) ‘Nia/Uakilifu wa Dhamira’ na (2) Mapenzi Mema kwa Watu wote Duniani.

‘Mapenzi mema’ na ‘Amani’ kwa watu wote Duniani ni kitendawili ikiwa jamii na wanajamii ‘hawajajitafuta na kujipata’ kulingana na muktadha akilifu wa usentienti, konsayansi na Ufahamu. Kwa

mintarafu ya hili, ‘Kujitafuta’ ni shughuli inayotaka ‘mabaharia’ waihakikishie jamii, chombo na wanachombo, Uhuru wa Kuamini/Kusadiki/Kuabudu ili kutia chachu ya Utu Bora na Kujichagulia. Basi ndiyo yawa, ili kuondokana na ukafiri, chombo hakina budi kuwa na lau ualama wa Ukumbusho wa Kuitafuta Nuru na Mwangaza Bora wa Utu. Kwa Tanzania, hili ndilo laja kwa utaasisho wa ‘Mwenge wa Uhuru’.

‘Mapenzi mema’ na ‘Amani’ kwa watu wote Duniani ni kitendawili ikiwa jamii na wanajamii ‘hawajajitafuta na kujipata’ kulingana na muktadha akilifu wa usentienti, konsayansi na Ufahamu. Kwa mintarafu ya hili, ‘Kujitafuta’ ni jambo la ‘mtu kupambana na hali yake’ na huku akijitafakari kwa kina yeye ni nani hasa duniani (?) Je, lipi ni kusudi hasa la yeye kuwepo Duniani? Basi ndiyo yawa, katika ‘kwesti’ ya kujitafuta mtu huishi kunyoosha ama/na kurunda mapito ya maisha yake. Kwa ufunguo wa Hekima-Umoja-Amani, mazingatio ya Wasafiri na Mabaharia ni Subira, Unyenyekevu na Utumishi. UTU wa mtu ni wenye thamani kubwa na tena wenye hitaji la kuchungwa vema ili kutoingilia ‘Uhuru wa Mtu’ katika makusudi yaliyo mema—mema ya nchi na watu/wanajamii ni fanusi ya rehema na fadhili inayotunza na kustahimilisha yote, yanayoonekana na yasiyoonekana.

‘Mapenzi mema’ na ‘Amani’ kwa watu wote Duniani ni kitendawili ikiwa jamii na wanajamii ‘hawajajitafuta na kujipata’ kulingana na muktadha akilifu wa usentienti, konsayansi na Ufahamu. Kwa mintarafu ya hili, ‘Kujipata’ ni hatma ya Imani na Kusudi la udhamirifu wa UTU bora. Kiufundi, Kujipata ndiyo kunakotamatisha ‘nia ya kujiwazia utu’--Yesu aliita hili kusudi ni ‘Kurejea Mbinguni kwa Baba’ ama pia ‘Ufalme Kuja Duniani’, mambo ya metafanusi ya Utu ilivyo ni UFAHAMU KRISTU. Basi ndiyo yawa, hatma ya ‘nia ya kujiwazia utu’ ni muktadha akilifu wa

‘KULIFAHAMU NENO’; mambo ya ‘NENO’ ndiyo lile khasa Buddha alifundisha kuhusiana na ‘Kauli Sahihi/Samma Vacha’.

‘Kujiwazia UTU’ ni Kutenda/Kuhuluku katika miili ya uweza na Roho ya Uzima Wote. Ontolojia ya ‘Ulimwengu Wote Dhahiri’ ni NENO—vitu vyote huanza na NENO na humalizika kwa NENO; ‘Kauli Sahihi/Samma Vacha’ ni ufunguo wenye kuona na (1) Umbonishaji Sahihi wa fahamu, (2) Uelewa Sahihi, na (3) Udhamirifu Sahihi wa UTU na MATUKIO—Matukio yategemeayo (1) Jitihada Sahihi. (2) Uisho Sahihi, na (3) Kitendo Sahihi.

Tanzania ni nchi iliyofanyiziwa kusudi la ‘Kujiwazia UTU’ bora ilivyo ni ‘Kuelekea Mashariki ya Sovereini Jumuifu’. Ujamaa uliondani ya mioyo ya Mabaharia walioasisi nchi-taifa ni ‘Sovereini Jumuifu’ na basi Maisha ni ‘Safari ya Kujitafuta’ kwa Uhuru-Udugu-Haki-Amani ambavyo mtu mmoja hapaswi kuhoji njia ya mwingine katika ‘kulitekeleza kusudi la udhamirifu wa utu bora’. Labda njia zote, kwa sura za dini na miongozo ya kiroho, huishia kumoja, lakini hili ‘fumbo la imani’ kwa wote—Wasafiri na Mabaharia; UJAMAA NI HAKIKA YA IMANI KATIKA NISHANI YA UTU BORA.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=cRVWy2YtJ7M>

=====

### **Nyota ya Utimilifu wa Miundo na Mageuzi**

Tanzania ni nchi iliyofanyiziwa kusudi la ‘Kujiwazia UTU’ bora ilivyo ni ‘Kuelekea Mashariki ya Sovereini Jumuifu’. Kwa mintarafu ya hili, Jaala ya Tanzania iko na ‘watu’ na ‘mioyo ya watu’ kama ‘Mbegu haradali’ ya ‘Mti Mkubwa Hasa’, mti wa kutoweza kudhaniwa kupata kutokea kwenye mbegu ndogo ndogo hasa --mti

wa Utamaduni na Ustawi wa Kimanyota; na basi, kheri ya Tanzania si hasa Utabiri wa/kwa ‘Nchi Fizikia’ ama/na ‘Utu wa Kibinadamu 1.0’. Tena basi yawa, Utanzania ni ‘ingilio tu’ la ‘Shughuli Pana’ ya Uanadamu na Matukio.

Wakati mmoja, mbele kiwakati, watu wa kusudi hili takatifu, wakifaulu mapana fulani ya kheri basi wataazimia taifa lao lenyekupata kuwa kitovu cha mageuzi makuu ya utamaduni na usivilai lichukue jina jipya—Nchi ya Watu Wakwanzania!

Safari yoyote huanza na hatua moja, na basi kuianza nia ya Utaifa--Taifa lililo na Mwangaza, Uhodari na Bidii ya kujifumua na kujifuma upya kunahitaji tu wale ‘Wateule’ wakumbuke, kujikumbuka na ili wapate Kukumbukwa. Kwa mintarafu ya hili, ikumbukwe vema, Tanzania ni Mwanzo wa Kuzaliwa kwa taifa jingine kubwa na lililo Jumuiifu—Taifa la ‘Umoja wa Mataifa Afrika! Tanzania ya kesho ni ‘jimbo la Wakwanzania’ Afrika...

Nchi nyingi za [Afrika huwa na Bendera zenye kuhusisha ‘Nyota’](#); kiuono na ufikirifu mifumo nyota ni ualama wa muktadha akilifu wa Utimilifu wa Miundo ya Mageuzi. Kwa mintarafu ya hili, Yantra Dhamma kwa mfano ni yenye Maduara yapatayo matano (5) ya muktadha akilifu kwa ‘mapenzi mema’--manne(4) ni ya ‘Dhamma’ na moja(1) ni la ‘UTUKUFU wa SURA ZOTE’ na utimilifu. Basi ndiyo yawa, ‘Nyota’ ni alama ya fahari ya UTU kutokea ‘Mbinguni’ – Bahari ya Yote. Kiufundi, duara la UTUKUFU wa SURA ZOTE ni kitovu cha mageuzi yote ‘pumzi za uzima na uweza wa kimiili’--asili ya ‘Eitha’. Ontolojia vya vitu vyote, na basi matukio yote ‘huanza’ na ‘kuishia’ na ‘Eitha’--‘Maji ya Mbinguni’; mwanzo wa vitu vyote kuumbika kwa sura na mfano wa Kile Kilicho ni Khasa ni ‘Uimajinishi wa Yote’ katika ‘UuMoja’; mambo ya jinesesia.

Yantra Dhamma, muakisiko wa fahari ya UTU bora kutokea kwenye kitovu cha ‘Maji yafanyayo Uzima wa Mbingu na Nchi’—na vitu vyote vinavyoonekana na visivyoonekana. Kwa mintarafu ya hili, Nyota ni alama ya utimilifu wa (1) Nchi, (2) Mbingu, (3) Upepo, (4) Moto, na (5) Eitha. Vitu vyote dhahiri, vyenye kuonekana na visivyoonekana vimeumbika kwa elementi tano ambazo hukadirisha ‘maduara’ na ‘vitovu’ vya maumbile/sura na Unishati—ilivyo ni asili ya supasha-wakati. Basi ndivyo yawa, Roho ya Uzima wote ni fumbo la Miundo na Mageuzi ya vyote na kila kitu katika hali ya kusitirika.

Mambo ya jinesesia, kiuono na ufikirifu mifumo, [ndiyo ile asili khasa ya ‘matukio’](#); kuumba/kuhuluku vitu ama mambo ya udhahiri ni kujiwazia ‘NENO’ la Unasaba wa ‘Miili ya Uweza, Pumzi na Uzima’. Kwa mintarafu ya hili, kile ambacho leo hii kinafahamika kama DNA ni unasaba wa kujiwazia UTU/KIUMBE. Kwa jinsi ya ‘Mwanadamu’ ama ‘KIUMBE’ cha sura na ‘utukufu’ tofauti na ‘binadamu’.

Nyota, kiuono na ufikirifu mifumo, ni muktadha akilifu wa UTU kwa mashahibiano ya ‘viungo kadhaa katika mwili mmoja’--miguu, mikono na Kichwa. Basi, kujiwazia UTU kunaweza kutendeka kwa NENO mahsusi la mwili wa kibinadamu lakini pia upo uwezekano wa ‘kujiwazia UTU’ kwa miili ya ‘Nguvu’ na ‘Uzima mwingine wa Ukiumbe-mtu’. Tena basi ndivyo kuwa, yule afahamikaye kama ‘Yesu’ ni mmoja wa ‘Waja wema’ wa ‘Utimilifu wa Miundo na Mageuzi’ kupitia miili ya uweza.

Mambo ya jinesesia, kiuono na ufikirifu mifumo, [ndiyo ile asili khasa ya ‘matukio’](#); kuumba/kuhuluku vitu ama mambo ya udhahiri ni kujiwazia ‘NENO’ la Unasaba wa ‘Miili ya Uweza, Pumzi na Uzima’. Kwa mintarafu ya hili, vyote vitatu (1) Maji Jinesesia, (2)

Fikara, na (3) Unasaba ‘DNA’ vina asili ya ‘Mwangaza wa Utu’ na ‘Habari za kufumia dhahiri’ ya Mwili/Miili ya uweza—‘Mwanadamu wa Nchi’ ama/hata pia ‘Mwanadamu wa Mbingu’.

Basi ndiyo yawa, kuna mengi ambayo ulimwengu na walimwengu wa leo wanataabika ‘kwa kukosa maarifa’--‘mwili wa nyama’ si ‘UTU’ wa mtu kwa kuwa hata mtu akikatika mguu, mikono ama hata kichwa ‘hafi’ bali mwili unaweza kufa ama kubakia hai kulingana na ukubwa ama udogo wa ‘uharibifu’. Siku za mbele, baada ya mafanikio ya kitekinolojia za kifizikia na metafizikia--hata mwili wote mzima wa mtu unaweza ‘kutibiwa’/‘kuponywa’/‘kufumwa upya’/‘kuotosheshwa viungo’, ikibidi, kwa kuuweka huo mwili ulioharibika katika mtambo-tiba unaoigizia na nururisha NENO la Uzima wa Mwili, mambo ya tekinolojia za Sayansi ya Eitha. tena kulingana na ‘Ugani Habari’ wa kujiwazia UTU wa Mtibiwa—jambo-tiba litakaloweza kuwa linatumia muda mrefu ama mfupi wa ‘kulazwa’ japo ni uhakika kabisa wa tiba/kupona/kuponywa.

Kujiwazia UTU ni muktadha akilifu wa ‘Kujitambua/kuwa na fahamu/Kuwa na hisia’ ambavyo (1) ‘unasaba’ na (2) ‘nuru ya uzima/mefanusi ya utu’; vinaweza kufanya/kutenda ‘kawaida’ ya uweza wa miili ya nyama na hata ‘zaidi ya kawaida’ kulingana na ‘Uelewa Sahihi’ na ‘Uakilifu Sahihi’ na basi ‘Udhamirifu Sahihi’. Kwa mintarafu ya haya, milango ya fahamu, na hususani ‘Macho’ vinawezesha muktadha wa imani, fikara na matendo ya kawaida na yanayopitiliza kawaida iliyozoeleka kutokana na ukweli wa fikra na uimajinishi vinamkaribiano wa udhamirifu, jitihada na matendo. Jicho ni mlango wa nafsi-roho ya mtu, kadiri pia DNA ya mtu ni ufunguo wa kipekee wa kudra na kheri za miili ya nyama. Basi ndivyo yawa, hata kwa (1) akili na (2) uimajinishi, na (3) Udhamirifu wa kuweka nia ya usikivu/masikilizano, [upo uwezekano](#)

wa mtu (1) ‘kupata fahamu’ kutoka ‘mbali ya upeo wa kawaida wa miili—kisupasha ama hata pia wakati’ na (2) ‘kutuma fikra/wazo/mawazo’ hata ‘mbali ya upeo wa kawaida wa miili—kisupasha ama hata pia wakati’, na (3) kupanga ama kupangua ‘matukio’ kwa ‘Sala na Ushawishi’ wa hata mambo yaliyo ‘mbali ya upeo wa kawaida wa miili—kisupasha ama hata pia wakati’.

Mabadiliko makubwa ya kitaasisi na Utamaduni barani Afrika yanakuja kutokana na uelewa, Uakilifu na Jitihada sahihi katika kudhamiria, kutenda na kuuishi usahihi wa mambo. Kwa Mintarafu ya haya, ELIMU 1.0, ELIMU 2.0 na ELIMU 3.0 vinahusika; Elimu 1.0 ni maarifa na ujuzi ujao na fahamu na mafikara ya juu ya mambo; Elimu 2.0 ni Uono na Ufikirifu Mifumo wenye kujinasibu mapana ama hata kina cha mafikara na tafsiri za mambo; na Elimu 3.0 ni ‘Ilimu ilivyo ni metafizikia ya Elimu’.

Elimu 3.0 ni ‘Ilimu ilivyo ni metafizikia ya Elimu’; ndiyo ugani wa maarifa na maarifu ya mambo—‘kujua kwa kawaida’ na ‘kujua kwa jinsi ya rohoni’ kwa alama, miongozo ama hisia/ujuaji usiyo wa moja kwa moja wa jambo/mambo. Ni kwa mintarafu ya haya, uono na ufikirifu mifumo unajipambanua hata kwa ujuzi wa lugha za binadamu ama hata ‘Malaika’. Basi ndiyo yawa, Ujenzi wa Nyumba, uendeshaji wa chombo na Ubaharia ni mambo yanayoweza kunasibika ‘Uganga/Ukuhani’ kwa ajili ya ‘Upatanisho’ wa mambo ya ‘Mbingu’ na ‘Nchi’; ama sivyo ‘maarifa ya kibinadamu, Elimu 1.0, hukadirisha ukomo wa mbinu, hadhi na hali za udhibiti wa sura na mienendo ya jamii kwa manufaa ya wachache katika upendeleo—upendeleo wa kimifumo ujao na ‘kuwa katika kujua’ kwa unahodha wa chombo.

‘Mwezi na Nyota’ na pia ‘Msalaba’ ndizo alama ufunguo kwa metafanusi ya ‘Ontolojia ya Taasisi’ yoyote kwa kuwa alama hizi mbili zinakutanisha muktadha wa ‘maarifa ya kibinadamu na malaika’. Kwa mintarafu ya haya, (1) Mwezi na Nyota ni asili ya Duara na Nukta—Mtanuko na Msinyao wa vitu vyote katika ‘ukuwa’ ama ‘ukuja kuwa’; na (2) Msalaba ni asili ya KUBU na Mageuzi. Basi muktadha wowote wa kujichagulia ni aidha mtanuko ama msinyao wa ‘Pumzi ya Uzima wa Miili’. KUBU ni kitovu cha upitilizi wa mtanuko na msinyao katika metafanusi ya ulimwengu dhahiri—mambo ya ‘Kumbukumbu la Miongozo’ na pia ‘Kumbukumbu ya Utaasisi’. Basi ndiyo yawa, katika ‘ILIMU’ kumbukumbu ni Shughuli ya ‘Malaika’--kuhakikisha yale yote ya ‘Kujiwazia UTU’ yanahifadhiwa msimamo wake na utukufu wake ‘Milele hata Milele’.

Kwenye Yantra Dhamma, ‘Mwezi na Nyota’ hujitokeza katika bega la kulia ya MRABA wa DHAMMA na Msalaba hutokea katika bega la kushoto. Kwa mintarafu ya hivi, UHURU na AMANI katika ALMASI YA NISHANI YA UTU BORA, kupitia ‘Muongozo Mbingu’ wa ‘LIBERTI’ ndiyo huzindika mapana ya ‘Unyoofu’ na ‘Mapenzi Mema’--muktadha akilifu wa topografu ya ‘Mwenge wa Uhuru katika kilele cha Mlima Kilimanjaro’. Basi ndiyo yawa, kila bega la MRABA wa DHAMMA lina pembetatu, za udhamirifu-jitihadamatendo, zilizositirika zipatazo sita (6); hizi ndizo zinazojitokeza katika ALMASI YA NISHANI YA UTU BORA kwa idadi ya nne(4) kila upande. Mkasi wa MRABA ALMASI na MRABA DHAMMA una pembetatu zipatazo arobaini (40); hizi hukadirisha unje ndani wa ‘Dodekahedroni’--kuingia na kutoka kwa udhahiri ‘maji-jinesesia-Eitha’.

Maumbo ya uyabisi Platofu, kiufundi, ni ile asili khasa ya ‘Duara’ na ‘Nukta’ kuegamisha ‘miundo’ na ‘mageuzi’; zipo yabisi Platofu

zipatazo tano(5) tu na ndiyo 'ile Tano' ijayo na pembetano za 'Nyota ya UTU'. Kwa mintarafu ya hili, ALMASI YA NISHANI YA UTU BORA ina pembetatu, za udhamirifu-jitihada-matendo, zilizositirika zipatazo kumi na mbili (12), tatu kila upande ilivyo ni katikati ya zile nyeupe. Hii ni idadi ya 'Watakatifu wa Kuhudumu patakatifu pa patakatifu' katika [baraza la KUBU ya NISHANI YA UTU BORA kwa vielelezo vya 'Malaika' wa 'Utume na Utumishi' wa dhamira za kujiwazia UTU](#). hizi hukadirisha unje ndani wa 'Oktahedroni'--kuingia na kutoka kwa udhahiri 'Upepo-Eitha'.

Kwenye Yantra Dhamma, 'Duara na Nukta' ni ile asili hasa ya 'Zabibu 13 za Kristu' katika vesika paisisi ya 'Duara Mapenzi' la Magharibi. Kwa mintarafu ya hivi, utonali wa hisia na kujisikia katika UTU ni fanusi ya 'Kristu kama Mpanzi'. Basi ndivyo yawa, duara zipatazo 13 zimejikusanya kukadirisha mpangilio alama ya 'Nyota ya Daudi', zikiwa na rangi rangi saba(7), kama ilivyo kwenye upinde wa mvua. Rangi saba ndizo zile khasa zinazofanya kanuni ya 'Oktavi ya Muziki', pia rangi za vitovu saba vya 'pumzi' kwa mhimili wa misokotano ya nyoka wawili wa utangamano wa kilogarithimu.

Katika Trizaniamu, alama ya 'Kujisikia' ndiyo alama pekee isiyokuwa na 'mistari' na hali maduara yote yanakadirisha vitovu vyenye uhusiano wa 'mistari-uunganishi minyoofu' na tena 'duara la utukufu'. Hili ndilo ile asili khasa ya 'Duara na Nukta' ya 'Utukufu wote'. Namba 13 ni namba ya Miundo na Mageuzi kwa 'fanusi Malaika'. Kwa 'Zabibu 13 za Kristu' na tena '[Tunda la Uzima](#)', maisha na uisho ni mawezekano kwa kudra za 'Uenye Enzi'. Basi ndiyo yawa, Tunda la Uzima, ni duara zipatazo kumi na tatu (13 ) zenye kuweza [kukamilisha uhifadhi wa yabisi Platofu zote tano \(5\)](#) na pia nasibu ya uwezekano wa 'Rizati ya Mageuzi ya Kisura/Miundo' kwa [MKIA-KUBU ndani ya fanusi METATRONI](#).

Kwa mengi yatokanayo na Yantra Dhamma na Trizaniamu, Afrika na Waafrika, wanao ufunguo wa miongozo kwa kheri na nafaka—kutia wepesi ‘Safari ya Kujitafuta’ katika mtu mmoja mmoja.

Ufunguo wa Miongozo kwa kheri na nafaka pia ni kwa watu wote Duniani, 2024 na kusonga, ili wapate ‘Uono Fasaha’ wa tathmini ama uyakinifu wa mambo na tena kwa ajili ya ustawi na ulinzi wa mifumo ya maisha—maisha katika nasibu ya mageuzi makuu ya miundo, utendaji na kujichagulia.

Katika haya, Tanzania ni ‘Nchi ya Ahadi’, si kwa kuwa fulani kasema hivi ama vile; bali ni kwa kuwa ule ufunguo kwa ajili ya ‘Nuru ya Ufahamu’ ni ‘Mwanzo wa Kutoka’ (Kutoka ni mageuzi ya kimuundo na utendaji jamii), tena kwa hiyari na Tumaini-Jema. Watu wa Tanzania, na tena watu wa Afrika wanao Uhuru wa Kujichagulia Jaala yao—ikiwa tu wanao upeo wa kuona ilivyobora: ‘mambo yenye kubana’ ,’mikingamo’ na basi kubaini ‘fursa iliyopo humo humo kwenye hayo mawili’ katika kuyakinisha mustakali wa maisha yao wao wenyewe.

Kiufundi, habari za kutegemea ‘Masiha’ kwa ajili ya ‘Ukombozi’ ama vipi imekuwa ni ujuzi na utundu wa kutekana fahamu kwa ajili ya ‘Tumaini’ na ‘Faraja’, labda mambo ya uongo na kweli--jambo hili ‘limepitwa na wakati’; katika zama hizi za maarifa kuongezeka na maendeleo makubwa ya tekinolojia ya habari na mawasiliano ‘Mwenge wa Uhuru’ unasafirishwa kwa habari fasaha na ufundi wa kubayanisha ‘fikra’ ama/na ‘alama’ za mashikizo ya jamii na utamaduni—kila mtu ‘atajibeba mwenyewe’; ikiwa atadanganyika ama kurubunika na ‘mifumo’ kwa kule kufikiri ‘Taasisi fulani’ itamkomboa hali yake kutoka kwenye uduni basi huyo ‘[Anaula wa Chuya](#)’ kwa [kujipendea yeye mwenyewe](#).

Mwenge wa Uhuru, ni ukumbusho wa raia, na tena basi wanajamii wote kufanyabidii kwa ajili ya kuimulikia mwangaza bora miundo yote ya utendaji kwa taasisi zao kwa kadiri vile vile ya wao wenyewe kutimiza wajibu wa kujimulikia nafsi zao kupitia usafi wa moyo na ‘Nuru ya Ufahamu’ iliyomo ndani ya viumbe vyote vyenye usentienti, konsayansi na ujifahamu.

Mwenge wa Uhuru, ni ukumbusho wa raia, na tena basi wanajamii wote kufanyabidii kwa ajili ya kuvimulikia mwangaza bora dhamira, jitihada na matendo yao katika jamii na taasisi—taasisi zinazofanya uzima wa mwili wa taifa na matendo yake katika nyakati za maisha. Moto wa mwenge ni alama ya ‘utakaso’ na ‘kuboresha hadhi/daraja la utu’; kundanisha upokeaji wa mwenge wa uhuru ni kushiriki kusudi la jamii moja yenye udugu, haki na amani kwa kuwa kusudi lenye kheri ni nishani ya utu bora.

Mwenge wa Uhuru, ni ukumbusho wa raia, na tena basi wanajamii wote kufanyabidii kwa ajili ya ‘kujitafuta’ mapana yaliyositirika ya ‘Kujiwazia Utu’ na ‘Uisho’. [Asiye na dhamiri thabiti ya ‘kujitafuta’ daima ni mtumwa wa pepo za mazingira na nyakati](#)--mifumo. [Moto](#) ni alama ya ‘[agano](#)’ na kile chenye kumuondoa mtu utumwani, ‘[Nyumba ya Misri](#)’/[Matriksi](#)—Moto, Nuru halisi ya UTU kutokea katika ‘[Uzabibu 13](#)’ za ‘Wazo UTU liliko Kuu’; ufaraguaji wa kaida ya ukumbusho wa ‘[Uwepo](#)’.

Basi kule Amerika ukumbusho wa dhamira, jitihada na matendo kwa ajili ya utu bora, matatu yajayo na ‘Kujiwazia UTU bora’, ndiyo yamefanyiwa sanaa ya ‘[Sanamu la Liberti](#)’, pale karibu na bandari ya New York. Nchi ya Tanzania imetaasishwa kuwa ‘nchi ya kimbilio’, [kiroho](#), kwa ajili ya shughuli ya ‘[Uhuru wa Afrika](#)’--Amani na Mapenzi mema Duniani kama vile Amerika ilikuwa ni kimbilio

kwa ajili ya ['nchi ya waliohuru'](#). Kwa Tanzania, mageuzi ya kimuundo jamii na wanajamii wenyewe ndiyo walengwa kuwa vinara wa Tumaini na Mapenzi mema—[yenye kupaswa kushirikishia watu wote duniani](#).

Kheri ya kundanisha ukweli wa 'Mwenge wa Uhuru' katika jamii yetu utakadirisha 'UTU-Binadamu MPYA'; Uafrika 1.0, Uafrika 2.0 na Uafrika 3.0. Uafrika 1.0 ndiyo huu tulioanza nao ambavyo tumechukulia mapambano dhidi ya 'nguvu za kudidimiza' heshima ya utu barani Afrika ni 'jitihada za mtu Mweusi' dhidi ya watu wa mataifa mengine Duniani—wasioyokuwa 'Weusi'.

Uafrika 2.0 ndiyo 'Shughuli' ya 'wadau' waliodhamiria na wanaodhamiria Afrika yenye Utu-binadamu bora pasipo kujali vigezo vya 'rangi ya ngozi'--[Mwalimu Nyerere na Washirika walioasisi taifa la Tanzania walilenga hili khasa katika kutaasisi nchi-taifa/Dola](#)—nchi changa yenye mseto wa watu wa makabila na rangi mbalimbali. Hili ni muhimu sana kwa 'Watanzania' kulifahamu, mambo ya nyakati na hali ilivyo kwa wakati hubidi namna ya mageuzi na taasisi ziwe 'zinajiongeza' kwa kusonga mbele na si kurudi nyuma.

Maendeleo yanayofanya Dunia kuwa kijiji yametutaka na kutubidi, sisi watu wa nchi ya Tanzania na hata Afrika yote kwa ujumla, tujifakari na 'kujitafuta upya'--jambo lenye kuwezekana kwa Elimu 3.0. Wakati mmoja siku si nyingi, kufika 2036, Dunia itakuwa na 'Uthibitisho' na 'Ujuzi' wa kutambua mambo ya UTU na Kujiwazia UTU kunakopelekea mtu kuzaliwa huku ama kule akiwa labda 'Mtu Mweusi'/'Mtu Mweupe'/'Mtu wa Bluu ama Mtu wa 'Namna Ingingine' kungine nje ya sayari yetu ya Dunina. Hili linakuja kwa Rizayati ya Elimu 3.0 na 'Tekinolojia za Kutekenya vishikizo vya Fahamu za

Mwili na Akili’. Kwa hivyo, Elimu 2.0 kwa wanajamii wote ni muhimu sana kwa kipindi hichi cha mpito kuelekea ‘Mafunuo zaidi’ ya ukweli wa mambo na muktadha uliositirika wa ‘Uzima wa Miili’.

Tanzania imekuwa na watu ‘Wateule’ wachache walioitengeneza njia na misingi ya ‘mageuzi/mapinduzi’ ya mifumo inatawala ‘Dunia ya Leo’ na hali, KWA SASA 2024, tupo kwenye kipindi cha ‘Lala Salama’, siku za mwisho za mifumo inayovuna ujinga na upoyoyo wa umma ambao haujazinduka. Basi ndiyo [amani ya dunia inalega lega na kupitia changamoto nyingi kwa kuwa ‘vita na machafuko huku na kule’ ni koroga koroga na kukorogana kwa ‘wahuni’ katika jamii](#) – jamii zilizo kwenye ‘mazingira hatarishi’ ama hata pia ‘zilizoendelea’; mambo ya ‘vipakazio’ vya kuepa mielekeo ya midololo wa kiuchumi na mifumo/siasa mbovu za tawala.

Tanzania Mpya na basi ‘Afrika Mpya’, Afrika 2.0, haiwezi kujitenga na madhila ya upepo mbovu wa kiuchumi, tawala na amani Duniani. Kusudi la kujihami na mambo haya, kwa Tanzania, lilitaasishwa kwa shughuli ya siasa za Chama cha Watu, Chama cha Wananchi—Chama cha Mapinduzi.

Haya yatukumbushe ukweli wa dhahabu, Afrika 2.0—Afrika Mpya, ni ushindi wa wanadamu wa sura na rangi zote. Mwalimu Kambarage Nyerere, alipodhihiri tamko la Chama cha Mapinduzi kuhusu dhamira na mwongozo kwa ajili ya kushirikiana ili kuleta ‘Haki na Amani’ Duniani, nia yake ilikuwa moja na ‘[Roho ya Ushindi](#)’:

**“Kazi ya Chama Cha Mapinduzi ni kuwaongoza Watanzania washirikiane na Waafrika wenzao kuleta uhuru na umoja katika Afrika nzima. Kazi ya Chama Cha**

**Mapinduzi ni kuwaongoza Watanzania washirikiane na binadamu wenzao kuleta haki na amani duniani; Chama Cha Mapinduzi ni Chama cha watu; Chama Cha Mapinduzi kitaongoza kutoka miongoni mwa watu na kitaongoza kikiwa ni sehemu ya Watanzania maana wananchi ndio waliokiunda Chama Cha Mapinduzi kiwe chombo chao na kiongozi wao”**

Mwenge wa Uhuru, ni shughuli ya kuchochea ‘Utaamuliko Jamii’ kwa ajili ya Afrika na Dunia Mpya—kupitia ‘UTU Mpya’; Mwanzo wa ‘Jua la Maarifu’.

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=Po2R9IbJCAE>

=====

## **Jua la Maarifu**

Imani ni safari kwa ajili ya Hakika ya UTU na Uisho.

Siku za zamani, [faraja ya Msafiri ni Dua yake na Imani](#), kwamba ijapokuwa akatiza katika ukonde wa uvuli wa mauti hatahofia Uovu.

‘Utaamuliko Jamii’ pia ni saga ya Msafiri; jamii inahitaji nguzo za imani kwa ajili ya safari yake ya matumaini – matumaini ya kuenenda salama.

Ijapokuwa jamii tofauti zimepata kufikiwa na miongozo ya kheri kwa ajili ya maisha na kuishi, jamii ya leo, tuseme 2024, bado inahitaji lile lile la ‘funguo za Maarifa’ kwa ajili ya kheri na salama ya maisha ya kileo.

Kiuono na ufikirifu mifumo, [safari ya kujitafuta kiroho ina hatua tatu](#) (1) Ya Nje, (2) Ya Mpito, na (3) Hatma ilivyo basi ni (A) Miongozo/Sheria, (B) Mbinu/vitendo imani, na (C) matunda ya kuiva na kukomaa kiroho. Kwa mintarafu ya haya, mambo ya nje ndiyo muktadha akilifu wa mapokeo ya kimila, desturi na sheria; mambo ya mpito ni muktadha akilifu wa 'kaida/sala/miditisha; na mambo ya hatma ni Utaamuliko, Kujitambua, Kuifahamu KWELI.

Elimu 1.0 inahusu 'Ya nje'; inaweza kusadifu mengi ya 'maarifa ama/na kujua' lakini kiufundi ni uelewa wa juu juu wa mambo. Elimu iliyotamalaki duniani—ya kuanzia chekechea hadi chuo kikuu, kiufundi, bado ni Elimu 1.0; inakidhi fahamu za mawazo na fikra kwa sura za juu juu lakini 'haina kina hasa' cha ukweli wa mambo... Hili ndilo linalotaka hata 'Maarifa ya Dini' yaje kujaribu kukamilisha 'kiu cha maarifa' ya Kweli.

Elimu 2.0 inahusu 'Ya Mpito'; ni njia ya hekima kwa kuwa Uono na Ufikirifu Mifumo ni shughuli ya kutangamanisha kinachojulikana na kile kisichojulikana pasipo 'Kasumba' bali 'Ushahidi' wa Muktadha Akilifu wa Ushahibiano wa Mambo. Hili ndilo linalotengeneza nasibu ya 'Kuipa Kina' Elimu 1.0 kwa yale yafahamikayo kwa ufasaha. Basi ndiyo yawa, Elimu 2.0 ni daraja la 'yenye ukomo' na 'yale yasiyo na ukomo' kwa kuwa 'mapengo ya maarifa/maarifu' daima yanakubalika; kilicho ni fumbo kinabaki kuwa fumbo na kinachojulikana kinayakinishwa kwa mapana, marefu na kina cha mashauri.

Elimu 3.0 inahusu 'Hatma'; ni hitimisho la mafikara na mwanzo wa '[Kuya-JUA](#)' yote. Kiufundi kuyajua yote, [ni uweza na upeo wa kutangamanisha yanayojulikana na yasiyojulikana](#) kwa 'Taamuli' na

‘Umbonishaji fahamu Sahihi’ wa mapana, marefu na kina ya mafikara/kujiwazia Utu—ili kupata kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wa ‘Uzabibu 13’, upitao ufahamu wa kawaida -- kwa jinsi ulivyo mwingi, kupata kutimilika kwa utimilifu wote wa kile kilicho ni khasa ‘Roho ya Uzima wote’.

Elimu 3.0 ni ‘Jua la Maarifu’--mwanzo wa kujua yote kwa jinsi ya ndani na nje ya dhahiri.

Elimu 1.0 na Elimu 2.0 ni ‘uwanja wa mafikara’ na hali Elimu 3.0 ni usikirifu na maarifu kwa siri za miundo/mageuzi na uzima wa miili. Kwa mintarafu ya haya, Elimu 3.0 ni ‘Maarifu’ ya halisia za ‘Mwezi na Nyota’ na pia ‘Msalaba’ wa fizikia na metafizikia ya mambo. Elimu 3.0 huleta madaraja ya nishani ya utu, kujichagulia na Matendo Makuu. Elimu 3.0 ndiyo ufunguo wa Ukamilifu wa Hekalu la Mwili—Mambo ya ‘Uimamu’ ama kusema ‘Uteule’ kwa huduma za kuongezea wengine njia katika ‘Safari za Kujitafuta Kiimani na Uisho’.

Katika ulimwengu halisi wa mambo, watu wa ‘Uimamu’ na ‘Uteule’ huandamwa na uhasimu wa ‘Mapokeo’ na ‘Taratibu’ kutokea kwa Wahifadhina wa hayo kwa kuwa, kiufundi, mapokeo na taratibu ni mambo ya usukaji miundo jamii kwa ajili ya ‘usawa wa kimashirikiano’; kuyatishia hayo usalama wake inaweza kuwa ni ‘msala’.

Miundo yote inayonasibu ya kubadilika palipo na ‘Nuru’/’Ujio wa Nuru’; kwa kuwa nuru ya ‘Jua la Maarifu’ daima husukuma ‘mageuzi’ ya utu na jamii’-- ‘ mwenye nuru’ na ‘jamii’ katika kukutana uso kwa uso. Basi, Nuru ya Mtu wa Daraja, huleta chachu

mpya ya utamaduni na kujichagulia ambavyo inaweza kuwa rafiki ama si rafiki na ‘hali ilivyo’/Statusi Kwou.

Na hili ndiyo adha iliyowakumba watu wa ‘Mwangaza’ katika nyakati na jamii mbalimbali; jambo linalotaka ‘[Mtu wa Mwangaza kuzicheza karata zake kwa uangalifu](#)’ kwa kuwa ‘kiza cha utu’/statusi kwou si rafiki kwa ‘Mvinyo Mpya’. Hili pia ndiyo daima limefanya [ulazima wa faragha](#) ama ‘sanaa ya kujichanganya na hali usijulikane’; kwa watu wa Elimu 3.0 kuishi hivi. Kwa hivyo, kiufundi, [watu wengi wa rizayati ya Elimu 3.0 wamekuwa ni walinzi wa ‘maarifa ya Kazi’ ya kuleta ‘Utaamuliko Jamii’ kwa ‘Subira’ na ‘Faragha’](#).

‘Maarifa ya Kazi’ ni upanga—ukiwa katika mikono salama, ni kheri ya ‘Haki’ na ‘Mapenzi Mema’ kuifikia jamii pana, kwa namna zinazofaa na wakati muafaka. [Ukiwa katika mikono isiyo salama, ni ‘mkosi’ wa ‘Madhalimu’ na ‘Dhuluma’](#)--mambo ya kufumbana ukweli wa mambo ili basi kutumiana katika mabatili ya ‘Kujilisha Upepo’. Kwa mintarafu ya haya, mambo ya faragha daima ni Utaasisi ndani ya Taasisi kwa kuwa Muundo wowote wenye kujishikilia kwa uadilifu wa mafikara/shauri, dhamira na matendo ni ‘Taasisi’.

Basi ndiyo yawa, si kwa kuwa kuna jumuiya inayodhaniwa kuwa na ‘faragha’ basi kuna nia ovu nyuma yake... Kuna namna hata ulimwengu wote umefanyika kwa mambo ya muktadha akilifu wa uwaziwazi na tena vile vile [muktadha uliyositirika](#)—jambo hili linalazimu uhitaji wa ‘[Roho wa Busara ya Utambuzi](#)’ kumaizi ni yepi ya kushiriki kwa kheri na kutoshiriki kwa kheri vile vile—mambo ya ‘kutotupia lulu kwa shuwaini’...

Katika kipindi hichi ya ‘Mavuno’, busara ni kutangamanisha yale yote ambayo yamejitokeza katika dini na miongozo yote ya UTU na kujichagulia--kuyatangamanisha kwa kusudi la ‘kuijengea jamii/jumuiya ya kimataifa uwezo wa kulivuka vuguvugu la upoteaji wa Amani na Tumaini’ Duniani. Hili linalazimu kulingania ‘Utaamuliko Jamii’ kwa minajili ya kuleta umahiri wa jamii yote nzima katika ugani wote wa Elimu 1.0, Elimu 2.0 na Elimu 3.0. Kuleta wepesi kwa jamii kutambua dini zote na mafundisho ya kiroho, hasa hasa yanayotawala idadi kubwa ya waumini, yana ‘Hazina’ ijayo ni ‘mafumbo ya Kiimani’ kwa ajili ya ‘Liberti’--kweli yenye kumweka mtu huru kweli kweli...

Kujengea jamii uwezo wa fumbua mafumbo ya imani kuna leta ‘kinga’ na ‘ulinzi’ dhidi ya migogoro inayoweza kuchochewa na ‘ujuaji wa juu juu wa mambo’--ujuaji mbovu unaoweza kuchochea dhamira, jitihada na matendo ya uhasama na machukizo dhidi ya ‘Ubinadamu’.

‘Shams al Maarif’, Jua la Maarifu, ni moja ya kompendiamu ya ‘Maarifa ya Kazi’ inayovutia wengi wenye nasibu ya Rizayati ya Elimu 3.0 na hali hapo hapo ‘inaogopwa’ na wengine wengi wasio na ‘msuli’ wa kuyakabili ‘Maarifa’ yake. Rizayati ya Elimu 3.0 ni uzao wa ‘shughuli za faragha’ za watu wa Maarifa na Maarifu. Katika mikono isiyo salama, huwa ni zana ya ‘Shetani’ na katika mikono salama huwa ni zana ya ‘Malaika’. Basi ndiyo yawa, katika ‘wakati muafaka’ ukweli wa hili hauna budi kuwekwa wazi ili kumalizana na ‘kasumba’ ama/na ‘nongwa’ ya ‘kujua mambo kwa sehemu’.

Hisia na Kujisikia ndiyo asili ya cheche ya ‘Utu’, ambavyo tena ni asili ya nukta na duara la utukufu wa ‘Roho ya Uzima wote’. Kiuno

na ufikirifu mifumo, hili linashahibiana na ‘nukta’ ya ‘andiko’ la (1)Kauli/NENO la kuanza yote kwa Jina la Rehema na Fadhili. (2) Kushukuru na Kutukuza ni ‘ombi’ la kijiweka sawasawa na ‘Mapenzi na Kheri’ ya kile kilicho ni asili ya Uzima wote na Amali zote za ‘Mbingu’ na ‘Nchi’. Kwa mintarafu ya ‘Mamlaka’ na ushahibiano wa Utaasi wa UTU na Utamaduni, asili ya yote hutajwa ni ‘Bwana wa Ulimwengu’.

Kiuono na ufikirifu mifumo, ‘Ufunguo wa Imani’ ni ‘Vesika Paisisi’ ya [‘Uzabibu 13’](#) ambavyo (3) Mbegu ya Miongozo ya Utu bora inakiriwa na kundanishwa(Rehema na Fadhili), (4) Utambuzi wa Utaasisi wa ‘Mtu/jamii katika Imani’ na hatma ya ‘Nyakati’ unakiriwa na kundanishwa (Eskatolojia—Siku ya ‘Hesabu’), (5) Kujisalimisha katika ‘Nishani ya Utu Bora’ – udhamirifu wa jitihada za kustahiki ‘kheri ya utukufu’ katika ‘Safari ya Kujitafuta’ (Sifa za kutosha Kuabudiwa kile kilicho ni Khasa asili ya ‘Mbegu ya Utu’ wetu kama ‘watu’, (6) Udhamirifu wa ‘Jitihada Sahihi’ kwa ajili ya kupata uongozeaji wa njia – njia za kujichagulia yaliyo na kheri ya ‘utimilifu wa kusudi la UTU’, (7) Udhamirifu wa ‘Kutumainia Mema’ na kuwa ndani ya ‘Mapenzi Mema’ ya fahari ya UTU.

Vesika Paisisi ni alama ya fumbo la imani kwa ‘mwanzo’ usiyokuwa na sababu/usababishwa; ndivyo yawa, uzima wote ni fumbo la ‘Uwepo’--ikiwa kile kilicho khasa ni khasa asili ya Uzima wetu ‘hakina mwanzo wala mwisho’--hakina asili ya ‘kuzaliwa’ wala ‘kuzaana’. Basi ndiyo yawa, [asili ya vyote vilivyodhahiri ni ‘Pumzi’ ya ‘Kimoja kisichogawanyika’](#). Tena basi, vitu vyote vimefanyika kwa ‘asili moja’ isiyogawanyika.

Yantra Dhamma ni Muktaadha akilifu wa Ujumuishii wa (1) ‘Fanusi ya Bwana (MRABA ALMASI)’ , na (2) Fanusi ya UTU(MRABA

DHAMMA). Kiufundi, Kuabudu ni (3) Fanusi ya ‘MAGEUZI KATIKA FAHARI ya NYOTA YA UTU’ kwa kadiri ya Rehema na Fadhili kile kimoja kisichogawanyika na hali ‘kimejaza Utukufu wake’ mbingu zote na nchi.

UHURU-UDUGU-HAKI-AMANI ni fanusi ya ‘Bwana wa Ulimwengu’; uhusiano wa MRABA WA BWANA na MRABA wa UTU ni (1) Swastika na ‘Mwezi/Nyota’ huwa na asili ya ‘Wakati, Nyakati na Matendo’, na (2) Mboni ‘AJNA’ na ‘Msalaba’ vina asili ya ‘[UONO METAFANUSI](#)’ juu ya ‘Hukumu’, ‘Hesabu’ na ‘kutangamanisha Mwanzo na Mwisho wa Vizio vyote vya Mambo/Miili ya Uzima. Kwa mintarafu ya haya, vitu vyote ‘huja na kwenda’ kwa ‘pumzi’--yale yote yasiyoendana na ‘pumzi ya asili’ ndiyo muktadha akilifu wa ‘Wale waliopotoka/potoshwa’, wakati mmoja wa ‘siku ya hesabu’, miili ya uzima katika metafanusi ya tuseme ‘UTU’ hupitia ‘moto’ kwa ajili ‘kufuta kumbukumbu’ ya ‘matawi ya mzabibu yasiyozaa’...

Kiuono na ufikirifu mifumo, [Uzabibu 13](#) katika Vesika Paisisi, ni muktadha akili wa (1) Nia ya Baba, ‘Bwana wa Ulimwengu’, na (2) Roho ya Uzima wote – Upendo Unaopitiliza mipaka yote ya ‘Dhahiri’. Kwa mintarafu ya hivi, Dhahiri yote ni ‘MWANA’--Utu na Kujiwazia UTU ni ‘Mawezekano’ katika ‘Mwana’. Basi ndiyo yawa, UTATU wa Baba, Mwana na Pumzi Takatifu ni kitu kimoja—ni ‘Uwepo’; Ni asili ya ‘MOJA’ iliyo ni vyote na kila kitu—Wakati ni ‘Maruweruwe’ katika muktadha akilifu wa usentieti, konsayansi na Ufahamu. Tena basi, ndiyo fasaha ya Buddha kuzungumza ya ‘Fadhaa ya Utu’ ni matokeo ya ukosefu/kuto kupatia ‘Kitovu’ cha kubaini ukatikati wa ‘Gurudumu la Dhamma’.

Kiuono na ufikirifu mifumo, kulia ya ‘Yantra Dhamma’ ni ufunguo wa muktadha akilifu kwa ajili ya ‘Matendo ya Imani, Kuabudu, Kujitoa Moyo na Muditisha’; Kwa mintarafu ya hivi, mambo kama vile (1) [Yoga Karma](#), (2) Kupiga magoti, kusujudia, kuinua mikono, kufumba mikono na kaida zote za ‘sala kwa ajili ya Upatanisho’, (3) [Yoga Bhakti](#), na (4) [Vipassana](#)—Jitihada kwa ajili ya ‘Samma Samadhi’ ; haya yote huleta ‘Utonali wa Hisia na Kujisikia’ ambavyo ‘chaji’ kwa ajili kufanyika ‘utu bora’ hukadirika kupitia ‘Roho ya Uzima’ wote.

Kiuono na ufikirifu mifumo, Jua la Maarifu ndiyo asili ya ‘Moto na Maji Jinesesia’ vifanyavyo ‘Mbingu’ na ‘Nchi’. Kwa mintarafu ya hivi, ‘Sala kwa ajili ya Upatanisho’ ni kustahiki ‘Rehema’ na ‘Fadhili’ ya kile kilicho ni khasa ASILI ya UZIMA wa MIILI YOTE—Yenye Kuonekana na isiyoonekana.

Basi ndivyo yawa, kupiga magoti na kufumba mikono miwili kifuani ni mkao wa unyenyekevu wenye muktadha akilifu wa ‘Swastika’; Kufumba mikono miwili mbele ya kifua kwa kuumanisha vidole ama kukutanisha nyuso za viganja ni muktadha akilifu wa ‘Vesika Paisisi’ ya ‘Ontolojia ya UTU’.

Basi ndivyo yawa, Kiuono na Ufikirifu mifumo, Kusimama(I), kuinama(Γ), kusujudu (--), Kukalia visigino(L), na vilevile kusimama huku kufumba mikono kwenye ‘Jua la Tumboni’ (+) ni matendo yenye muktadha akilifu wa ‘Unje-Ndani wa Msalaba’ ambavyo [Mapana na Marefu](#) ya MRABA DHAMMA yanaakisika. Tena basi, ‘[Swala Tano](#)’ ndiyo asili khasa ya ‘Fahari ya UTU ilivyo ni Nyota’--Kuswali mara tano kwa siku ni ‘Nguzo’ ya ‘Imani’ kwa ‘Nishani ya UTU Bora’ ambavyo UTU ni ‘Mwezi’ wa ‘Gurudumu la Dhamma’--‘[Jua la Tumboni](#)’ na ‘[Jua la Kwenye Paji la Uso](#)’ ndiyo

khasa vitovu viwili vya Mageuzi ya Kiutu kwa 'NIA YA UZIMA'. Kiufundi, nia ya uzima, ndiyo huleta 'Unyoofu wa Kusudi' katika 'Mapenzi na Utukufu' katika 'Kujiwazia UTU'--Kujiwazia UTU katika 'Metafanusi ilivyo ni mambo ya 'Jicho la Upaji/Mboni 'AJNA' katika kaida ya Kusujudu.

Vitovu viwili vya Mageuzi ya Kiutu kwa 'NIA YA UZIMA', Kiuono na ufikirifu mifumo, ndiyo khasa asili ya 'KUBU na MAGEUZI'. Kwa mintrafu ya hili, Fralektori ya Musa ni muktadha wa 'Yantra Dhamma' ambavyo pia 'NISHANI YA UTU BORA' inakusudika kwa 'kaida na matendo' ya Sala—Utumwa, Kutoka, Misri na Kumbukumbu la Ahadi na 'Nchi ya Ahadi' vyaifanya nguzo ya Imani ya Kiyuda. Basi ndiyo yawa, kiuono na ufikirifu mifumo, (1) Hijja, (2) Kuznguruka Kaaba, na (3) 'kumpiga mawe shetani' ni muktadha akilifu kwa (1) Koherensia ya Udhamirifu wa 'Safari Moja ya Kujitafuta' kwa wale walio amini, (2) Jitihada za 'Kukusanya Pumzi ya Kupaa Mbinguni', na (3) Kuyakataa mambo yanayoshikilia ama/na kuchelewesha 'Fanusi ya Nishani ya UTU Bora' isijichagulie 'Wongofu Mkuu'.

Kiuono na Ufikirifu mifumo, KUBU ni kitovu na mageuzi, kujichagula na Udhamirifu, ndivyo basi katikati kabisa ya 'Yantra Dhamma' kuna 'KUBU ya Mistari Miekundu' itokanayo na fanusi ya 'Nyota ya Daudi'. Kwa mintarafu ya hivi, Umbonishaji Fahamu sahihi katika kitovu cha Yantra Dhamma ni Ufunguo wa Maarifu—Maarifu kwa ajili mageuzi, kujichagulia na Udhamirifu wa UTU BORA. KUBU ya Yantra Dhamma ni kipatanishi cha 'NYOTA ya FAHARI ya UTU' na kujiwazia UTU. Maarifa ya Siri za Mbingu na Nchi yanawezekana kwa Umbonishaji Fahamu Sahihi na 'Sala/Ombi' kwa ajili ya 'Kufanyika Mtu Mpya/Mtu Bora/Mtu wa fahari ya Mbingu na Nchi.

Kiuono na Ufikirifu Mifumo, kitovu cha Yantra Dhamma ni ‘Nukta’ ya ‘Kufanyika na kutofanyika’ kwa yote. Kwa mintarafu ya hili, Yantra Dhamma ni ufunguo wa ‘Uholografia wa Kikwantumu’ wa yote yaliyo Dhahiri kwa Kuonekana na kutoonekana. Yantra Dhamma ni kadiri ya kujengea koherensia ya unishati wa yote kuchukua muundo/sura na vile vile ‘kuja na kwenda’ kwa ‘Pumzi’ ya ‘Roho ya Uzima’ wote. Kila mtu, kile kiumbe chenye Usentieti, Konsayansi na Ufahamu kinaweza yote kwa utambuzi, kujitambua na kutambuliwa katika ‘Roho ya Uzima’ wote—Iwe ‘Mwanadamu-Mtu’ ama ‘Malaika-Mtu’, iwe ‘Mwanadamu-Simba’ ama ‘Malaika-Simba’, ‘Mwanadamu-Mdudu’ ama ‘Malaika-Mdudu’ n.k kwa kuwa ‘Umalaika’ ni ‘Metafanusi ya Ulinzi na Upatanisho wa Mambo ya Mwanzo na mwisho wa pumzi za Kujiwazia Utu’.

Metatroni, Kiuono na ufikirifu mifumo, ni Metafanusi ya Utu na Kujiwazia UTU ambavyo ‘Ubindamu-Mtu’ unaweza kujipambanua ‘Mbawa zake’ katika ‘Pumzi ya Miili ya Uzima ya UTU’--mapana ya ‘wakati na usiwakati’ vyenye kukadirisha kufanyika na kutofanyika kwa Kujiwazia UTU wenyewe. Kwa mintarafu ya hivi, ndivyo basi husemwa ‘Enoko’ alitembea na Mungu/Miungu/Malaika hata ‘Mbingu ya Sita’; kuiona Mbingu ya Saba ya Utukufu na Enzi ikiwa na ‘Kiti cha Utukufu wa Enzi’ chenye ‘Ukaribu wa Malaika Metatroni’ mwenye ‘Kutumikia’. Kwenye Yantra Dhamma, Nyoka wawili wakadirishao ‘vishawishi’ na ‘kujichagulia’ huishia kukazia macho kitovu cha sita cha ‘Pumzi ya UTU’--kitovu cha ‘Mboni AJNA’. Basi ndiyo, ‘Kusali/Kuomba/Kuswali/Umbonishaji Fahamu Sahihi ni kwa ajili ya kuvizidi ‘vishawishi’ na ‘majaribu’ kwa ajili ya ‘Wongofu’; Mbingu ya Saba, ambamo ‘Mbegu ya Kujiwazia UTU imesitirika’ kwa ajili ya ‘kufanyika na kutofanyika’ kwa yote na vyote.

Kiuono na ufikirifu Mifumo, Maisha na Kuishi ni Mseto wa ‘Mafikara-Meta’ ya ‘Uzima wa miili yote’. Kila kilichodhahiri kinaishi na kudumu ndani ya ‘Pumzi ya Kingine’ chenye ‘Uzima Zaidi’. Kwa mintarafu ya hili, ‘(1) Umeme na (2) Chaji ya Miili ya Uzima’ ndivyo huwa asili ya ‘Uweza, Nguvu na Utukufu’--Majua, Sayari na Kosmosi ya ‘Umoto/Baridi’ kudumu katika kuzungurukana, kujizungurusha na kusongambele katika mapana yasiyo na mwanzo wala mwisho ya Usupasha-wakati.

Kiufundi, miundo, matendo na mageuzi ni (1) ‘uelekronishi’ wa (2) ‘fikara/sakiti umeme’ na (3) ‘Ufahamu/Ugani wa Usumaku’ kukadirisha dhahiri ya ‘mbingu’ na ‘nchi’.

Kila kilichofanyika ni ‘Pumzi’--pumzi ya ‘Chaji-Umeme’ ya ‘Uzima/Usumaku-Umeme wa Yote na vyote’; basi ndiyo vile, kadiri ya kile kilichofanyika kuvuta/kupuliziwa pumzi na kutoa pumzi/kutolewa pumzi, vile vile kujikusanyia ama kutapanya chaji yake, hili hukadirisha (1) uzima wa miili, (2) miundo na mageuzi ya Sura vile vile (3) ‘Uweza, Nguvu na Utukufu’. Jua na Sayari ni zenye umbo duara/tufe kwa kuwa ‘[Uzabibu 13](#)’ huanza na kumalizika hivyo katika ‘Metafanusi ya Uzima wote’; basi ndivyo kadiri ya ‘fikara’ lolote, kuwa ni ‘Ontolojia ya Taasisi’ kwa muktadha akilifu wa nukta na Duara (Nguvu ya Utendaji wa Umeme-Sumaku).

Kiuono na ufikirifu Mifumo, Maisha, Kuishi na Riziki ni Rehema na Fadhili za ‘[Uzabibu 13](#)’. Kwa mintarafu ya hili, ‘sala na kazi’ ni imani na hakika kwa yale yatarajiwayo. Basi ndivyo yawa, lile shauri la ‘Uzao wa Mzabibu’ na muktadha akili wa uisho katika ‘[Hali ya Neema](#)’. Kiufundi, Neema, ni ufunguo ilivyo ni ‘[Gongo kwa Msafiri-Zaburi 23](#)’ ambavyo ‘Moyo wa [Shukrani](#) na [Kutukuza](#)’ hukusanya ‘chaji zaidi wa kusukia uzima wa miili’ hata kuweza kudhahirisha

‘mageuzi ya Ujazi’. Ahadi ya ‘Uzabibu 13’ ni ‘Kaa ndani yangu, Nikae ndani yako—Akaaye ndani yangu huyo huzaa Sana!’ Basi ndivyo yawa, Liberti na Ujazi ni matunda ya ‘Unyoofu’ na ‘Mapenzi Mema’ kwa mwanajamii kwenye kujichagulia fungu la kupata katika ‘Uweza, Nguvu na Utukufu’ wa ‘Ujulikano wa Mtu’ katika ‘Roho ya Uzima’ wote.

Kiuono na ufikirifu Mifumo, Maisha, Kuishi na Riziki ni Rehema na Fadhili za ‘Uzabibu 13’. Kwa mintarafu ya hili, ‘Kutoa Zaka’ ni muktadha akilifu wa ‘Ibada’ – ushirikiano kwa ‘Mema ya Nchi’ na ‘Fadhili’ katika jamii kwa kusudi la kutengeneza nguzo ya Imani ya ‘Nishani ya UTU Bora’. Kiufundi, Zaka ni Utakaso wa ‘Undugu’ na ‘Haki’--Kwenye Mapana ya Kusini ya MRABA wa DHAMMA. Basi ndiyo yawa, Zaka ni Chachu ya ‘Umbonishaji Fahamu sahihi’ wa ‘Dhamma’ na ‘Gurudumu la Dhamma’ pia kadirisho wa ‘mambo ya nyakati’; na tena muktadha akilifu wa ‘mapana ya jamii’ yenye wale ‘waliongozewa vyema katika njia ya Haki’ ama ‘kupotoka’.

Waliongozewa vyema katika njia ya Haki’ ama ‘kupotoka’, katika ‘Nyakati za Sasa’ ndiyo shauri la hukumu ya ‘Jua la Maarifu’ kwa ajili ya ‘Mavuno’--majilio ya UTU wema Duniani.

Mifumo ya Maisha ambayo inamuundoa mwanajamii katika kusudi la ‘Nishani ya UTU Bora’ ni ‘Upotofu’-- wa Kuongozwa na ‘Yule Muovu’; na mapelekeo ya Muktadha akilifu wa metafo ya ‘Shetani’.

Kiufundi, wema ama/na uovu ni ‘tafsiri’ za uakilifu wa kawaida wa mambo—katika metafanusi ya mambo hakuna uzuri ama ubaya khasa kwa kuwa kile kinachotia nguvu kizuri, hutia nguvu kibaya vilevile. Tofauti ya kimapelekeo ya tafsiri kwa ‘Chema’ na ‘Kiovu’ ni ustahiki wa ‘Rehema na Fadhili’ za ‘Roho ya Uzima Wote’ ambavyo

‘Wema HAUFI/hauozi’ na hali ‘Uovu HUFA’. Uovu huishi kwa ‘kuibia pumzi’ ya kile kilichokatika mapana na marefu ya ‘mtu’ wa ‘UTU katika Uzabibu 13’ – mtu aliyebado katika safari ya kujitafuta.

Basi ndiyo yawa, wema na ubaya ni mapelekeo yasiyoepukika ya nasibu ya ‘Utashi’ na ‘Kujichagulia’. Tena ndivyo basi, mtu wa mwangaza kusema “hakuna mwema ila yule mwenye kumulikia 'Mwangaza wa Jua' na tena 'Kunyeshea Baraka ya Mvua' wote -- wema na wabaya...” ni kushuhudia ‘Hekima ya Roho ya Uzima Wote’ inayopitiliza ujuaji wa juu juu wa mambo—ujuaji wa juu juu katika ‘mtu aliyebado katika safari ya kujitafuta’.

SASA, haya yote yanahusu vipi na ‘Jaala’ ya taifa la Tanzania?

UHURU-UDUGU-HAKI-AMANI ni mambo yajayo na ‘Hekima’ na ‘Mapaji ya Roho’ ilivyo ni majilio ya ‘Tumaini-Jema’ la Maisha na Uisho wa UTU bora. Kwa mintarafu ya hivi, ELIMU 2.0: UONO NA UFIKIRIFU unayonasibu ya kuleta Mageuzi Makuu ya Miundo ya Utendaji wa Kijami, Mazingira na Usivilai.

**‘JUA LA MAARIFU’** kwa Taifa la Watanzania ni **MWANZO-KUTOKA-HESABU-UKUHANI-KUMBUKUMBU YA MIONGOZO** kwa ajili ya ‘MTI WA UZIMA’ wa Afrika, Dunia na Walimwengu wote.

**MWANZO:** Ni Kheri sana, Jamii ya Watanzania ikafanyiza ndani ya ‘Akili na Moyo’ ule Udhamirifu, Jitihada na Matendo kwa ajili ya ‘JUA LA MAARIFU’; Uhuru-Udugu-Haki-Amani ni ‘Makumbusho’ kwa ajili ‘Nia na Marejeo ya Misingi ya Nchi na Tawala’.

ELIMU ELIMU ELIMU ndiyo ufunguo wa umaizi wa ‘Nishani ya UTU Bora’ kwa ajili ya Kulijenga Taifa la Wanajamii ‘Wanaojielewa’ na kufanyika uwezo wa kufahamu Ontolojia ya Taasisi zifanyazo na kukadirisha ‘Umadhubuti’ ama ‘Uzorotaji’ wa kusudi la kuelekea ‘UJAMAA’ wa Kweli—Sovereini Jumuifu.

**KUTOKA:** Ni Kheri sana, Jamii ya Watanzania ikafanyiza ndani ya ‘Akili na Moyo’ ule Udhamirifu, Jitihada na Matendo kwa ajili ya ‘KUJISAHIHISHA KITAASISI’; Marejeo ya Nia na Misingi ya Nchi na Tawala yanawezekana ikiwa kuna ‘Uono Fasaha’ na ‘Sahihi’ juu ya Mifumo, Miundo ya Utendaji na Upeo wa kumaizi ‘Mazingira yasiyo Rafiki kwa Ustawi wa Umma’.

Mageuzi ni kuondoka kwenye Mifumo KUBU Nyeusi ya kuwashikilia wanajamii na ‘Mifumo ya Kibabiloni’ ili kuitekeleza azma ya ‘UHURU’--Uhuru wa Kweli wa Mtu/Jamii/Taifa na Mataifa.

Yantra Dhamma na Trizaniumu ni zana za Ufunguo kwa ‘Elimu’ na ‘Fahamu’ ya ‘fizikia na metafizikia’ ya Jamii—Hili ni la ulazima kuzingatiwa, kwa karibia wanajamii wote; ikiwa tungalipenda ‘Mageuzi’ yasiwe ni Nira ya kufungiwa ‘Wanaoamini’ na ‘Wasioamini’.

**HESABU:** Ni Kheri sana, Jamii ya Watanzania ikafanyiza ndani ya ‘Akili na Moyo’ ule Udhamirifu, Jitihada na Matendo kwa ajili ya ‘TAASISI NA UTAASISI’ unaotimia kwa mgawanyo wa majukumu, idadi ya watu na Uhitaji wa Taifa/Mataifa. Maendeleo huja na Uskani wa Gurudumu la Maisha unahitaji wanajamii wawe hai kwa wito na majukumu yao kwa wao wenyewe pia Taifa/Mataifa.

Studio Maendeleo ni Taasisi kwa ajili ya Utaasisi wa ‘Maendeleo ya UTU na Vitu’; ikiwa jamii inafanya vizuri katika ‘Utaamuliko Jamii’ basi Mageuzi na Maendeleo Bora yatakuja huku yakileta Hesabu ya mabadiliko ya Sura na Hali za wanajamii kwa minajili ya Makazi, Uchukuzi na Mazingira.

Kiufundi, mahitaji ya mwanadamu huakisi uhitaji wa ‘Uwepo’ kwa ajili ya ‘Chakula, Malazi na Mavazi’--Kazi ni kutekeleza wepesi wa maisha kwa ajili ya mtu/jamii/wanajamii kuweza (1) kuwa hapa namaa pale kiwakati ‘Makazi’, (2) kuzitumia rasilimali zake na kuzifikisha penye uhitaji ‘Uchukuzi’, na (3) Mazingira rafiki kwa kuwa haya hukamilishana na shughuli zote za mwanadamu/mwanajamii.

Kimazingira, watu ni rasilimali, hili ndilo linalolazimu hasa ‘Utaamuliko Jamii’ kwa kuwa ‘Taasisi na Utaasisi’, kiuono na ufikirifu mifumo, ni muktadha akilifu wa ‘mazingira ya miundo, utendaji na kujitengenea’. Kwa mintarafu ya hivi, ili muundo wowote na utendaji wake kuwa thabiti huhitaji wanajamii ama/na watendaji wawe na ‘Mwangaza wa Kutosha’ wa kujipangilia, kujiendesha na Kujitathmini.

Gurudumu la Dhamma ni mapelekeo ya jamii yenye mwangaza kwa ajili ya uyakinifu wa UTU wake—jambo lisilo na asili na miundo ya kipiramidi, miundo ya wachache kuamua hatma za wengi kwa kuwa mifumo ‘inauma’ na ‘kupuliza’ kwa choyo, uwizi na ubinafsi—choyo, uwizi na ubinafsi uliohalalishwa na ‘Matriksi’ na tena kwa janja janja ya ‘Elimu za Mchongo’.

**UKUHANI:** Ni Kheri sana, Jamii ya Watanzania ikafanyiza ndani ya ‘Akili na Moyo’ ule Udhamirifu, Jitihada na Matendo kwa ajili ya ‘HAKI YA MBINGU NA NCHI’; Taasisi zote zina mafungamano ya ‘wakati na usiwakati’ kukadirisha ‘Mifumo’. Kwa kadiri nchi-taifa/Dola ni ‘Taasisi’ ni wajibu wa kila mwanachi ‘Auchunge Wakati’ ama sivyo atalazimika ‘Kuukomboa Wakati’.

Basi ndivyo yawa, Wakati ni ‘Rasilimali’ ya kifizikia na pia Metafizikia – pasipo fahamu na ufahamu sahihi, mwananchi/mwanajamii anaweza kujikuta ni ‘Mtumwa wa Maombi’ kwa ‘Mungu Anayepotezea Maombi’ ama ‘Kutotabirika muda wa kuyajibu hayo Maombi’.

Uelewa Sahihi wa Fizikia na Metafizikia ya Jamii, kwa kila mwanajamii, ni hitajiko mujarabu ili Maarifa na Maarifu ya ‘Jua la Maarifu’ lilete pambazuko la UTU bora ilivyo ni ‘Utaamuliko Jamii’. Kwa mintarafu ya hili, itashangaza lakini ndiyo ukweli wa mambo; katika ‘Hekima ya Roho ya Uzima wote’: Kusudi la Dhahabu ni “Kuutafuta Ufalme wa Mbingu na Haki yake, ili mengine yazidishiwe humo humo...”

**KUMBUKUMBU LA MIONGOZO:** Ni Kheri sana, Jamii ya Watanzania ikafanyiza ndani ya ‘Akili na Moyo’ ule Udhamirifu, Jitihada na Matendo kwa ajili ya ‘KUSUDI TAKATIFU LA NISHANI YA UTU BORA’. Uhuru-Udugu-Haki-Amani ni ALMASI ya NISHANI YA UTU BORA. Kiufundi, kuiishi Nishani ya UTU bora ni kuwa ‘Nuru na Chumvi’ ya Duniani.

Mwenge wa Uhuru juu ya Mlima Kilimanjaro ni Kuiweka Taa juu ili imulike kote—ilete ‘Utaamuliko wa Jamii’; Vivyo hivyo, Udhamirifu

wa Utu wema ni kuwa ‘Chumvi’ ya ‘Utamaduni’ na ‘Usivilai’ wenye Tunu kwa Mataifa mengine yote.

Na basi ujumbe ufuatayo unawahusu wanajamii wa Tanzania, kama asemavyo ‘Mtu wa Mwangaza na Katika Uangaza Wenyewe’:

*“Ninyi ni chumvi ya Dunia; lakini chumvi ikiwa imeharibika itatiwa nini hata ikolee? Haifai tena kabisa, ila kutupwa nje na kukanyagwa na watu. Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji hauwezi kusitirika ukiwa juu ya mlima. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya pishi, bali juu ya kiango; nayo yawaangaza wote waliomo nyumbani. Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.”*

=====

<https://www.youtube.com/watch?v=-qTXwKFbOl8>

===